# Majina Ya Makufuru

Asante, Ndugu Neville. Jambo hili lilikuwa kwa namna fulani la—la kustaajabisha kwangu. Sikutegemewa kuwepo hapa leo; bali usiku wa leo ni usiku wa Ushirika, nami—nami niliona ningeshuka nije asubuhi ya leo. Basi nilimpigia simu Ndugu Neville, naye akasema, "Vema sasa, kama unashuka kuja," kasema, "mbona usituzungumzie kidogo."

Nami nikawaza, "Vema, kama ningeshuka, na iliwezekana, sitakuwa nikihubiri, bali ningalitaka tu kuzungumza na kanisa kidogo juu ya mambo ambayo, mwajua, ambayo nafikiri yangeliliimarisha kanisa."

Tumerudi hivi karibuni kutoka kwenye ninii yetu—kutoka kwenye mawindo yetu ya msimu wa mwisho wa mwaka (mimi na hawa ndugu hapa), nasi tulikuwa na wakati mzuri mno pamoja na...Tunashukuru sana. Sote tulishiba na—na—na tukapata wanyama pori tuliokuwa tunawinda. Na—nami pamoja na mchungaji wetu tunajua ya kwamba nyama ya kulungu ni nzuri sana, sana. Na kwa hiyo, tulikuwa na kulungu wazuri. Nami nilipata dubu na kulungu wawili.

Ndipo tukarudi, na huu unapaswa kuwa ndio ule wakati ninaopaswa kuzungumza juu ya zile Muhuri Saba za mwisho. Nao hawakumaliza kujenga kanisa. Na kuna kitu, kizuizi, ambacho kimesababisha jambo hilo, ambacho...Nafikiri hili jiji linatupa wakati mgumu, kwa sababu ya kutokuwa na nafasi ya kutosha ya kuegeshea magari kwa ajili ya wingi wa watu ambao tuna—ambao kanisa litaenea.

Tunataka kanisa jipya lijengwe hapa, na tuna kiasi cha fedha cha kutosha kilichokwisha kutengwa na—na kwa ajili ya kujenga ka—kanisa kubwa zaidi. Bali tunapokuwa na ibada hizi, mbona, mnafahamu ni nini. Ni jambo la kusikitisha sana: watu wamesimama kwenye kuta, huko nje kwenye mvua, na—na—na ni jambo baya sana. Na hata shutuma hutoka kwa marafiki zangu, likasema, "Ndugu Branham, inaonekana kana kwamba wao..."

Daktari fulani rafiki yangu alisema, "Inaonekana kana kwamba ungalipata mahali fulani ambapo unge-... ninasikitika," kasema, "...nipitapo."

Nesi fulani jirani yangu alisema, "Mbona, nilipitia kule alfajiri moja kwenye saa 11. Ulikusudiwa kuwapo pale," kisha kasema; "watu tayari wamekusanyika kwenye hilo kanisa hapo kwenye saa 11 alfajiri. Ulikuwa uwe pale kwenye sasa 3:30." Kwa hiyo, mnaona? Na inalifanya kuwa jambo gumu.

Nasi tunataka kanisa ambalo lina nafasi, na mahali ambapo kila mtu anaweza kuketi chini. Nasi tunafikiri tunaishi katika siku za mwisho—tunaamini kwamba—kwamba mahali ambapo ninii—tunapaswa kuwa tukifundisha kanisa juu ya—juu ya mambo haya yanayokuja: mambo ambayo yametabiriwa, baadhi yao, maelfu ya miaka; na kwa yapata miaka ishirini na mitano na thelathini moja kwa moja katika kanisa hili, ambayo yamekwisha tabiriwa yangetimia. Na sasa, tunayo yakija kutimia moja kwa moja. Kwa hiyo tunapaswa kuwa tukifanya upya mambo haya, bali hatuna nafasi ya kutosha.

Kwa hiyo asubuhi ya leo. . .Ningeninii, nikipiga simu zangu na kadhalika jana, nami nikapata ninii—wengine kufanya alasiri ya leo na kadhalika. Halafu basi, nilikuwa na ninii—watu waliotaka kuingia: jamaa mdogo ambaye ana ugonjwa wa fadhaa, ndugu mhudumu hudumani; na lo, wengi wa namna hiyo; na ndugu fulani kutoka Norway. Nasi—nasi tulikuwa na mahojiano madogo kule nyuma kwenye chumba cha nyuma, nami nikasema, "Vema sasa, tutatoka tu nje."

Naye Ndugu Neville akasema, "Vema, tungetoka na kusema mambo machache ya kulihuisha kanisa kidogo."

La kwanza—moja ya mambo ya kwanza ambayo nataka kusema. . .Niliandika mambo fulani hapa kwenye karatasi, ili nifikapo kanisani, nilitaka kusema. Jambo moja nililokuwa nimeandika lilikuwa kuhusu kuaga dunia kwa Ndugu Taylor tulipokuwa tumeondoka.

Ndugu Taylor alikuwa anahudhuria kanisa hili kwa miaka na miaka. Sote tulimjua, nina hakika. Bali kama kungekuwa na wageni hapa, ilikuwa ni yule mzee muungwana ambaye daima alikutafutia kiti cha kuketi, Ndugu Taylor. Mara ya mwisho niliyomwona, naam, mpaka nilipomwona nikiwa kijana, alikuwa anasimama pale mlangoni yapata Jumapili tatu ama nne zilizopita. Akasema, "Ningetaka kuchukua vitabu, Ndugu Branham. Ningetaka kuvisambaza vitabu hivi."

Kwa hiyo sisi. . .Yeye. . .Ninavyofahamu mimi, alikuwa ana kisukari akazirai na haku-—bila kujua alikuwa na kisukari—naye alikuwa. . .Akafa. Hakufa; alienda tu kuwa pamoja na Bwana Yesu.

Naye alikuwa ndugu mwaminifu na wa ajabu, daima akiwajali watu wengine. Na furaha yake ilikuwa kujaribu kumtafutia mtu fulani mahali pa kuketi walipokuja kanisani. Nanyi mwajua, labda tutakapovuka kwenye ile nguzo, si litakuwa jambo zuri kumwona Ndugu Taylor, kule, akitutafutia mahali pa kuketi kwenye ng'ambo ya pili?

Nafikiri katika kumkumbuka Ndugu Taylor. . .Sikuweko humu kuzungumza kwenye—pamoja na Ndugu Neville kwenye

mazishi yake, bali nataka kutoa rambirambi zangu kwa mjane wake. Dada Taylor, nadhani, yuko hapa mahali fulani asubuhi ya leo. Nautakia heri moyo wake mwaminifu.

Ndugu Taylor, siku moja alisema, “Panda uje kunisalimu. Ninalo bwawa dogo lililochimbwa kule. Niliweka samaki wachache mle kwa hiyo ungekuja ukavue samaki.” Daima alimjali mtu mwingine, na kulikuwa na Mtu fulani aliyemjali yeye; huyo alikuwa Kristo, kumpa wokovu. Nami nafikiri kwa ajili ya kumbukumbu ya kanisa hili, linapokusanyika kama mwili mmoja tena asubuhi ya leo, na tusimame pamoja na kuinamisha vichwa vyetu mbele za Mungu.

Baba yetu wa mbinguni, sisi kama wanadamu asubuhi ya leo na—na wanaohudhuria mahali hapa pa kuabudia... Mkono Wako mkuu umetenda kazi miongoni mwetu na kumwondoa kwetu mmoja wa ndugu zetu wa thamani, ambaye tunampenda na tunajua ya kwamba Wewe ulimpenda. Nawe ulikuwa na sababu kwa ajili ya haya yote, Bwana, la sivyo haingalitukia namna hii, tukijua ya kwamba Biblia yetu inatwambia ya kwamba mambo yote hutendeka kwa manufaa ya hao wanaompenda Mungu; na hilo alifanya.

Nasi tunaangalia kila mahali ulimwenguni, na tunaona ma—maumbile, kwa kila njia, yakitwambia ya kwamba kaburi haliwezi kumzuia, kwa kuwa duniani alitimiza kusudi ambalo ulimtuma humu kutimiza. Alikuwa ndugu mzuri na mwaminifu.

Nasi tunaona ya kwamba katika uhai wa maisha ya mimea, na katika maisha ya jua ambalo huchomoza asubuhi kutupa nuru... Na mchana linafikia umri wa makamu, halafu, jioni linakufa tena, kisha linafufuka tena asubuhi inayofuata likiwa changa na jipya, kwa maana lilitimiza kusudi la Mungu.

Tunaona maua yanapochanua, na kuipamba nchi, na kuzipamba kumbi za mazishi na sehemu za kufanyia arusi, na kutumikia kusudi fulani: likifungua moyo wake na kutoa kwa moyo mkunjufu, asali kwa nyuki, na manukato kwa mpitaji, na uzuri kwa anayetafuta; linatoa yote liliyo nayo kwa ajili ya utumishi wa Mungu, kisha linainamisha maskini kichwa chake. Bali majira ya kuchanua yajapo linainuka tena, kwa kuwa lilitimiza kusudi la Mungu.

Halafu mbele ya maumbile yote, na Biblia, ile Ahadi, na Roho Mtakatifu, tunaweza kufurahi moyoni mwetu kwa kujua ya kwamba Ndugu yetu Taylor, vivyo hivyo, Bwana, alitimiza kusudi la Mungu. Basi kusema kwamba yeye hatafufuka tena ingekuwa ni kuikana Biblia, Mungu wetu, na mambo yote ambayo Mungu ametupa kuangalia, kujua ya kwamba kuna kufufuka. Kwa hiyo tunautazamia wakati ambapo tutamwona tena, wakati yeye ni kijana na mwenye afya na hatakuwa mgonjwa tena wala kuzeeka.

Mbariki mke wake wa thamani, huyo mwenziwe mwaminifu. Jinsi tutakavyowakosa kwa muda mrefu, Bwana, tunapowaona wakienda pamoja kwenye kile kidimbwi, na wakiketi kwenye zile mbao za kukalia kule, wakivua samaki na kuzungumza, na jinsi walivyokuwa wanapendana.

Basi sasa, tunajua ya kwamba kuna siku kuu inayokuja wakati wale mashujaa wa imani watakapopita wakitembea chini ya tao kuu la ushindi, nao Malaika wa—wakiwa na nyimbo za sifa watajaa hewani. Tutawaona tena mahali pale.

Hata wakati huo, Bwana, tupe ujasiri. Tubariki na utusaidie. Tutamkosa Ndugu Taylor, na kila mmoja anayekuja kwenye kanisa hili, jinsi angesimama mlangoni na kutafuta mahali kwa ajaye kusikia Neno la Mungu, apate kuketi amestarehe na kupumzika.

Na hivi majuzi wakati alipoaga dunia, Bwana, niliomba ya kwamba Malaika Mkuu wa Mungu aliyesimama pale mlangoni kumtafutia mahali pia, Bwana, ambapo angeweza kuketi chini. Kwa maana imeandikwa katika Biblia, "Wenye rehema watapata rehema." Mpaka tutakapomwona, Bwana, jalia ile kumbukumbu iendelee kuwa tamu mioyoni mwetu, mpaka siku moja tutakapokutana tena kwenye ile nchi nyingine. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

Yeye atakosekana kwa muda mrefu kati yetu sisi na miongoni mwa wageni na kadhalika wanaohudhuria kanisa letu ama jengo letu hapa kuabudu. Nafsi yake na ikae katika amani mbele za Mungu hata siku ile. Siku moja pia, kila mmoja wetu ataondoka mmoja mmoja, mpaka tutakapoingia mstarini namna iyo hiyo. Hebu nasi sasa, wakati tuna wakati na tunaweza, na tujitayarishe wenyewe kwa ajili ya wakati ule ujao; kwa kuwa hatujui itakuwa lini. Hatujui ni nani atakayefuata. Na tuishi ili kwamba kila siku, ya kwamba kama huo utawahi kuja, utakuwa kwa ajili yetu, tutakuwa tayari.

Sasa tungetaka kutoa matangazo. Sasa hivi karibuni, huenda ikawa labda. . .Sijazungumza na wadhamini tangu niliporudi, kuhusu hali ya kujenga ka—kanisa hapa, ama tunachopaswa kufanya baadaye juu ya kupata kanisa letu kusudi tuweze kufanya mikutano yetu. Kisha nitaendelea (samahani) na zile—zile Muhuri Saba. Halafu, kuna vile Vitasa Saba na—na mambo mengi bado ambayo yatupasa kuyaingilia mara moja.

Na sasa, Jumapili ijayo asubuhi huko—ninapaswa kuwa Elizabethtown, Kentucky, pamoja na Ndugu L. G. Hoover, kwenye ibada ya kuweka wakfu. Na hiyo ni kuweka wakfu maskani mpya—ama maskani ambayo wamenunua kule Elizabethtown, Kentucky: moja kwa moja kwenye ya 62 hata utakapofika Elizabethtown—ama moja kwa moja kule chini—

namaanisha ya 31, ama kule chini kwenye kituo cha kodi ya barabara. Kwenye tu mahali pa kugeukia inakupeleka mpaka Elizabethtown. Ni kama saa moja; ni kama maili thelathini na tano, arobaini kule chini. Nafikiri yapata maili arobaini kwa njia ya—ya 31, na yapata maili thelathini na tano ama kitu kama hicho kwenye ile njia nyingine, ukishuka kwenda karibu na kituo cha kodi ya barabara. Iko kwenye Barabara ya Mulberry. Ile ibada ya kuweka wakfu. . .

Ndugu Hoover atakuwa na shule ya Jumapili ya kawaida saa 4, nami ninapaswa kuhubiri ibada ya kuweka wakfu kutoka saa 5 hadi saa 6, Jumapili hii ijayo, Novemba 11.

Kwenye ubao wa matangazo kule nje kuna—ni tangazo lake, na itakuwa kwenye. . .Unaweza kupata njia kutoka papo hapo. Yako kwenye Barabara ya Mulberry, ama wao—wao wanatoa maelezo kwenye. . .Yako kwenye ubao wa matangazo kule nje mbele ya kanisa.

Halafu mnamo—mnamo ta—tarehe 22 Novemba, i—inanibidi kuwa Shreveport, Louisiana, kwenye tarehe 22, 23, 24, 25, na 26—siku tano, nafikiri, huko Shreveport, Louisiana, kwenye Maskani ya Uzima. Hiyo ni pamoja na Ndugu Moore. Wao wanasherehekea sikukuu ya ukumbusho wa mwaka wao wa hamsini. Baraka za Pentekoste zilishuka huko Shreveport, Louisiana, miaka hamsini iliyopita, tarehe 22 ya mwezi huu. Miaka hamsini, ujumbe wa kwanza wa Kipentekoste ulihubiriwa, na kushuka—Roho Mtakatifu alishuka Louisiana. Nao wana ukumbusho wa jambo hilo, na huu ndio ukumbusho wa mwaka wa hamsini. Nami ninapaswa kuhubiri yubile hii, siku tano usiku pamoja na Ndugu Moore kule Shreveport, Maskani ya Uzima.

Kama mna marafiki karibu na kule, mbona (ambao mnataka kuwaandikia ama cho chote kile), tungefurahia kuwa nao kule. Basi waambieni tu juu ya hiyo mikutanao ijayo.

Nayo Maskani ya Uhai, endapo mtu ye yote amewahi kuwa kule pamoja na Ndugu Moore, yeye ni mtu mzuri sana. Pia kuna kundi la watu wazuri sana. Hao wa Kusini wa tangu siku nyingi, ni vigumu kuwashinda. Na kwa hiyo, Maskani ya Uzima, ye yote aliye karibu na Shreveport anaweza kukwambia mahali ilipo. Shreveport ina karibu watu 200,000, na ni mji mzuri na kuna malazi mengi, kwa hiyo. . .

Nayo hayo maskani ni maskani makubwa, maskani makubwa sana. Yana orofa, roshani, na sakafu ya chini, na halafu sakafu chini yake; na kuna nafasi tele kweli, na moja kwa moja upande wa pili wa—kutoka kwenye ukumbi wa jiji ambao unakaa watu elfu tano—kama—kama tu kuvuka barabara hapa kwenda kwenye ukumbi wa jiji.

Naye Kasisi Jack T. Moore ama—ama aidha Maskani ya Uzima kule Shreveport, Louisiana. . . Hiyo inaanza tarehe 22.

Hiyo itakuwa Alhamisi hadi Jumapili: Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili, siku nne badala ya tano, nasikitika. Hiyo ingekuwa tarehe 22, 23, 24, na 25 (nafikiri hivyo ndivyo ilivyo) ya—ya Novemba.

Halafu, tutaona basi vipi kuhusu—kile tumefanya kuhusu kanisa hapa, tuone jinsi kanisa limeendelea juu ya kupata jengo lake. Makandarasi wanatwambia wanaweza kuweka watu wa kutosha katika shughuli hiyo, mpaka yapata karibu siku kumi wanaweza kulitayarisha hivi kwamba tunaweza kuingia ndani yake. Mnaona? Upesi sana. Nao wanangojea tu jiji litie sahihi... Mwajua, nasi tunapaswa kuwa na kiasi fulani cha mahali pa kuegeshea magari, kiasi fulani cha *hili*; na loo, jamani, ni kupitia mambo mengi rasmi, kabla ya kuanza kujenga cho chote.

Lakini ningetaka kufika kanisani kabla sijarudi hudumani tena. Naam, nina mwito kwenda Tanganyika, Uganda, na kupitia kule. Joseph ametayarisha mikutano itakayoanza Februari.

Na jana nilipoingia, kulikuwa na baadhi ya ndugu na Dada Toms na hao wengine kutoka nchi za ng'ambo waliokuwa wamekuja, nami nilikuwa—nilipata kijikaratasi mlangoni mwangu—ama—ama mwaliko kutoka kwenye shi—shirika moja kule Afrika Kusini. Kwa hiyo ninawaandikia kuona tu linaloweza kufanywa. Labda nitakapokuwa umbali huo, ninaweza kwenda Afrika Kusini, labda, kwenye sehemu ya mwisho ya Februari na Machi mnamo wakati huo.

Nasi tunakusudia kulijenga kanisa, kusudi niweze kuingiza hizi Nyakati za Kanisa kabla—kabla majira ya kipupwe hayajaanza, ikiwezekana. Kama haiwezekani, ama inaponibidi kurudi kutoka kule, kama Bwana Yesu akikawia...

Nilikuwa nikisikiliza jana nilipokuwa ninachukua—naamini ilikuwa ni juzi—kwenye kanda. Nilifikiri niliisikia ikicheza hapa asubuhi ya leo. Maskini ndugu fulani wa Kusini alikuwa... Mama yake alikuwa amehudhuria mkutano; alikuwa na ugonjwa wa kufisha kwenye titi lake, naye alikuwa ametiwa uvuli wa mauti. Ndipo Roho Mtakatifu, katika mmoja wa mikutano ya hivi karibuni kule—Southern Pine, naamini ilikuwa huko, ama mahali fulani, alimwambia, kasema juu ya ugonjwa wake wa kufisha, na Yeye alikuwa ni nani, na alikotoka; kisha kasema alikuwa na mvulana aliyekuwa amerudi nyuma, naye angepata ajali kisha ashtakiwe kwa mauaji yasiyo ya kukusudia, na mambo mengi sana ya namna hiyo.

Basi huyu jamaa... Yote yalitukia tu vile... Na ugonjwa wake mbaya sana wa kansa—au kivimbe cha kufisha, hasa, ulimwacha (ambacho, kivimbe cha kufisha ni kansa, mwajua).

Kwa hiyo basi kili—kilimwacha, na mvulana wake alikuwa ameshtakiwa kwa mauaji yasiyo ya kukusudia, na kila kitu jinsi Roho Mtakatifu alivyosema. Naye aliongozwa kwa Kristo—akarudi tena. Naye akafanya kanda yake, nami—nami niliisikia ikicheza. Hivi mlifurahia hayo mazungumzo madogo ya Kusini? Kasema, "Hapa chini North Caroliner. . . ," akasema. [Ndugu Branham anaiga kukokoteza sauti kwa ndugu huyo wa Kusini—Mh.] Loo, ninapenda tu jambo hilo sana, hao watu wa Kusini. Naye alikuwa. . .Bwana ndiyo kwanza ambariki kwa jambo hilo. Kasema, "Najua unasema huhubiri fundisho, Ndugu Branham, ila kwa kusanyiko lako tu," kasema; "sisi ni sehemu ya kusanyiko lako." Kwa hiyo hilo lilikuwa jambo zuri sana kwake kusema hivyo.

Basi sasa, kuna picha. . .Nafikiri labda ipo kwenye ubao wa matangazo asubuni ya leo. Kama haipo, Billy ataiweka kule. Mara nyingi imesemwa, nilipoanza kuzungumza hayo wao walisema, "Unawazia tu, Ndugu Branham, ya kwamba unaona Nuru hiyo, ile Nuru."

Labda ni vigumu. . .Huenda ikawa kuna wengine waliosalia hapa, watu wa zamani ambao wanakumbuka kule nyuma, kabla picha Yake hata haijawahi kupigwa. Kuna ye yote hapa ambaye anakumbuka mimi nikisema jambo hilo, muda mrefu sana uliopita? Angalieni! Yapata tu mikono minne ama mitano: Dada Spenser hapa, na Ndugu na Dada Slaughter, na—na Ndugu hapa, Ndugu kule. Kuna tu kama watano ama sita wa wale wa zamani waliosalia.

Vema sasa, baada ya kitambo kidogo, jicho la mitambo ya kamera ile lilipiga picha ile. Kwa hiyo ikaenda Washington, D.C., kisha ikapitia kwa wachunguzi halafu ikarudi, na ha—hakuna kupigwa picha mara mbili wala cho chote kile. Kasema, "Nuru iliguza lenzi." Huyo ni George J. Lacy. Mnayo sahihi ya jina lake. Mnaona?

Vema basi, mara nyingi unasikia, naangalia kule nje na kusema, "Kuna kivuli cheusi juu ya mtu huyu. Ametiwa uvuli wa mauti." Ni wangapi wamenisikia nikisema jambo hilo mara nyingi (mnaona?), mara nyingi? Vema, ilitukia kwamba kamera ilishika jambo hilo. Na kwa hiyo tunayo hiyo hapa.

Mwanamke fulani aliyemjia dada fulani na alikuwa amemwambia katika mkutano kule—kule Carolina, ambako tulikuwa na mkutano mzuri sana kule Southern Pines. . . Na kule, yule bibi alikuwa akifa kwa kansa iliyokuwa kwenye matiti yote mawili. Nao madaktari walikuwa wamemkatia tamaa wamemwacha afe. Ndipo yule bibi alinyosha mkono na kumpiga picha mara tu nilipokuwa nikimwambia alikuwa nani na mahali alipotoka; nami nikasema, "Kuna kivuli cheusi juu yako. Umetiwa kivuli cha mauti." Naye yule bibi akapiga tu picha ya jambo hili, na hiyo pale kwenye. . .Jicho la kimitambo la kamera limekipiga picha kivuli cha mauti.

Kuna mmoja wenu ameona ile *Amri Kumi* na kuona malaika wa mauti, jinsi alivyoingia, kile kivuli cheusi kinachoonekana cha huzuni? Kiko kwenye picha hii. Nami nafikiri iko kwenye ubao wa matangazo sasa. Kama haiko, Billy anaweza kunisikia, mbona, mwambieni aiweke kwenye ubao wa matangazo. Nayo ina mshale unaoelekeza kwa huyo mtu. Naye huyo mtu. . .Hicho kivuli kilimwacha huyo mwanamke na. . .akaponywa kimiujiza. Lakini kuna kama kifuniko cha moshi mweusi kilichomzunguka na kufanya kifuniko juu ya huyo bibi, na kikining'inia juu ya kansa hiyo, namna hiyo, kikitoka kwenye hicho. Bila shaka hicho ni kivuli ambamo mauti inatiririkia ndani yake kutoka kwenye ile kansa.

Vema, haidhuru ni jinsi gani unavyojaribu kuwaambia watu kweli, kuna mtu fulani atakayekuwa na shaka kwamba si kweli. Na iwapo daima unasema kweli, basi unajua wewe—wewe u sahihi.

Nina rafiki ambaye ni m—mfugaji kule Magharibi. Na—na Hifadhi ililipa yapata $4,000 kwa ajili ya gari la barafu kuhesabu kundi la kulungu wakubwa waliosalia huko kwenye Bonde la Troublesome. Bw. Jefferey, aliyeketi humu kanisani, nilimwongoza kwa Kristo—kafiri kwelikweli. Nanyi mmenisikia nikisimulia hadithi ya sisi kupanda farasi pamoja. Naye hakuamini ya kwamba—hakuamini kitu ila maadili ya Darwin, na yule Mtoto Mchanga, aliyezaliwa na bikira, ilikuwa ni upuuzi. Nasi tulipiga kambi pale pale hasa alipompokea Kristo.

Na kwa hiyo basi, mtu huyu akamwambia; akasema, "Sasa, mimi—si lazima ununue gari hilo—gari hilo la barafu." Kasema, "Nitakwambia ni kulungu wangapi hasa walioko kule." Kasema, "Kuna kumi na tisa." Kasema, "Kulikuweko na ishirini—kulikuweko na ishirini na mmoja, nami nikaua wawili wao." Naye alikuwa anazungumza na mlinzi wa wanyama pori. Hupaswi kuua ila mmoja. Kwa hiyo akasema, "Kulikuweko na ishirini na mmoja, nami nikawaua wawili. Wanasalia kumi na tisa."

"Naye akasema, "Naam, Jeff, najua uliua wawili."

Akasema, "Niliwaua!"

Vema, wakachukua gari la barafu wakapanda wakaenda kule, na kulikuwa na kulungu wakubwa kumi na tisa. Akasema, "Billy, mwambie tu mtu kweli; hataamini." Kwa hiyo hivyo tu ndivyo ilivyo. Unaweza kuwaambia watu kweli, na hata hivyo wao. . .Kumekuweko na kutoelewa kwingi sana na—na kusema uongo kuhusu mambo, mpaka wao hawaamini ya kwamba unasema kweli wakati unapowaambia kweli. Mnaona?

Lakini tunashukuru sana ya kwamba tuna Baba wa mbinguni ambaye huthibitisha Kweli hiyo kwa uthibitisho. Ni

Kweli. Kwa hiyo basi, kama hii itakuwa siku yangu ya mwisho duniani, ile. . .Hata utafiti wa sayansi na mathibitisho yamethibitisha ya kwamba nimesema kweli kuhusu mambo haya. Hiyo ni kweli; ni kweli. Kwa hiyo labda itakuwa kwenye ubao wa matangazo. Billy, umo humu chumbani humu? Unayo mkononi mwako, ile picha? Na iwapo unayo, basi ilete hapa, halafu unaweza kuiweka hapa, nao labda wanaweza kuiona. Vema, sijui. Kutakuweko na nuru kwenye—kwenye ubao.

Na hii hapa ile—hii hapa ile picha papa hapa. [Ndugu Branham anaonyesha ile picha—Mh.] Nadhani hamwezi kuiona, bali papa hapa mnaweza kuona kile kifuniko cha kivuli cha mauti juu ya kichwa cha mwanamke yule. Na hapa kuna maandishi juu yake huku nyuma, ambapo yule bibi alipiga ile picha na—kuona kama kweli ilionyesha; na hiyo hapo ku—kule. Ni kifuniko cha kivuli cha mauti. Mnakiona juu ya yule. Umekiona nadhani. Ndugu Neville?

Kwa hiyo Billy labda ataiweka kwenye ubao wa matangazo, tafadhali. Billy atakuja aichukue, na kuipeleka kule upande wa mbele, na kuiweka kwenye ubao, ili kwamba kila mtu aweze kuiona wanapotoka nje. Yeye ama Doc, mmoja wao. Sasa, nilifikiri labda ingeweza kuonyesha dhahiri vya kutosha kwamba mngeweza kukiona, bali kuna giza jingi sana kwa picha ya namna hiyo. Bali ataiweka kule ili kwamba mpate kuiona mnapotoka nje.

Sasa, kumbukeni matangazo yote.

Na sasa, asubuhi ya leo nilifikiri labda kwamba tungezungumza kwa muda kidogo juu ya kitu fulani kulitia moyo kanisa, kitu ambacho kingewapa ninyi ni—ninii zaidi. . .

[Ndugu Branham anazungumza juu ya tochi na ndugu yake, Edgar—Mh.] Naam, Doc, kama ukiweza. Huenda ikawa ni zuri. Nataka kutumia hii hapa. Nilikuwa. . .Wengine wao hawakuiweka kwa ajili ya juma lililopita, kwa hiyo tukafikiri labda ingetoa vizuri zaidi kwa leo. Nilitaka kuzungumzia jambo hilo, kwa maana linahusu ndo—ndoto aliyoota dada fulani.

Sijui kama Dada Shepherd yuko kanisani asubuhi ya leo. Nilikutana naye juzijuzi usiku. Na mara yangu ya kwanza niliyopata kumwona huyo mwanamke. Kweli, hata sikujua alikuwa ni nani. Je! yeye. . .? Nadhani yeye si. . .Naam. Tafadhali, lingekuwa jambo baya kama nikirejea kwenye ndoto hiyo? Dada Shepherd, usingejali sivyo? Vema, ni sawa. Na kabla hatujaliendea jambo hilo, na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tena.

Baba wa mbinguni mwenye rehema, Kwako tunatoa sifa kwa wema Wako wote na rehema. Na sasa, tutulize, Bwana, kusudi tupate kulisoma Neno la Mungu Aliye Hai, kama linavyotujia katika ono na linathibitishwa na Roho Mtakatifu,

huku likiungwa mkono na Biblia. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Wewe utatupa ufahamu, kusudi tupate kujua la kufanya katika siku hizi za mwisho tunapoziona nguvu za uovu zikituzunguka sasa. Vile vita, vile vita vya mwisho, viko karibu sana kupiganwa. Tusaidie, Bwana. Kama mashujaa halisi, wenye nguvu, na tuiinue ngao ya imani juu pamoja na Neno la Mungu, ule Upanga, na tupige hatua kwenda mbele. Katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, tukiwazia juu ya kusonga mbele, kwa vita, kama vi—vita vilivyoandaliwa, tayari kupiganwa, vita ha—halisi kupigana vita vya imani . . .

Dada Shepherd, hapa, na Ndugu Shepherd, ambao ni rafiki wetu wazuri sana, na ambao wanahudhuria maskani hii . . . Nao ni watoto wa thamani wa Mungu. Basi—basi huyu Dada Shepherd . . . Nilipokuwa nikichukua barua zangu (ambazo Billy anaweza kujibu, zile za mtu kusema tu, "Nitumie leso kadha za maombi." Nami huziombea; yeye anazijibu tu. Bali ikiwa ni barua ya kibinafsi, sina budi kuijibu mimi mwenyewe. Mnaona?) . . . Kwa hiyo nikachukua barua zangu za kibinafsi. Na kwa hiyo nilikuwa nikizichukua kwenda nazo nyumbani, nami nilikuwa nikisoma mle; ilisema, "Kutoka kwa Dada Shepherd." Nayo ilikuwa ni ndoto aliyokuwa ameota miezi kadha iliyopita. Naye asingeweza kuifahamu mpaka Jumapili mbili ama tatu zilizopita wakati nilipofundisha juu ya hizi—hizi *Nyakati Saba za Kanisa* na—na yale—yale matunda saba—2 Petro, jinsi inavyopasa ku- (2 Petro 1)—kuongezea kwenye imani yetu. Mnaona?

Kwanza: kimsingi, ni imani. Pili: tia kwenye imani yako, nguvu: kwenye nguvu zako, maarifa; kutoka kwenye maarifa, kiasi; kutoka kwenye kiasi, saburi; kwenye saburi, utauwa; na kutoka kwenye utauwa, upendano wa ndugu—wema wa ndugu; na halafu upendo ukiwa ndio jiwe la kufunika juu—saba ya mambo hayo. Nyakati saba za kanisa (mnaona?), na nyota saba za nyakati saba za kanisa, na zote hizo zinachanganywa pamoja na Roho Mtakatifu.

Sasa, hayo ndiyo yanayohitajika kuwa mtumishi wa Kristo. Kristo hulijenga Kanisa Lake katika nyakati saba za kanisa, Bibi-arusi Wake, Mtu fulani, Mwanamke, Kanisa. Nyakati saba za kanisa zinamuumba na kumfanya Bibi-arusi: wengine kutoka kwenye wakati *huu*, na wengine kutoka kwenye wakati *ule*, na wengine kutoka kwenye wakati *ule*, na wote pamoja, na kuliumba Hilo kama piramidi.

Kama vile Henoko alivyojenga zile piramidi, ambazo tunaamini . . . Na jiwe la kileleni kamwe hakikuwekwa juu ya hizo, kwa maana jiwe la kichwani lilikataliwa.

Na tunalichukua sasa, si kama fundisho, bali ili kufahamu, kwa ajili tu ya kanisa hapa, ili kwamba hawa . . .

Mungu hujifanya Mwenyewe mkamilifu katika tatu. Hujifanya mkamilifu katika Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, afisi tatu za Mungu mmoja. Hujifanya mkamilifu katika Kuhesabiwa Haki, Kutakaswa, Ubatizo wa Roho Mtakatifu; zinakuwa kazi kamilifu za neema. Yeye hujifanya mkamilifu katika kuja kutatu: mara ya kwanza kumkomboa Bibi-Arusi Wake, mara ya pili kumpokea Bibi-Arusi Wake, mara ya tatu katika ule Utawala wa Miaka Elfu pamoja na Bibi-arusi Wake. Na kila kitu hukamilishwa katika *tatu-tatu*. Na *saba* ni namba ya Mungu ya ibada; Mungu huabudiwa katika *saba*, kumalizika. Sasa imekamilika na imemalizika.

Na jambo la ajabu lilikuwa (si kuingiza jambo hili, bali kuwaonyesha tu), kulungu wa mwisho niliyempata alikuwa na ncha tano upande mmoja na tatu kwenye ule mwingine (mnaona?): neema na ukamilifu.

Sasa angalieni juu ya jambo hili, ya kwamba Kristo… Mungu aliandika Biblia tatu. Biblia ya kwanza ilikuwa angani, inayoitwa zodiaka. Naam, kama hujui kitabu cha Ayubu, sahau hilo, maana—kwa maana Ayubu ndiye anayelielezea: jinsi alivyoangalia juu, kisha akavipa majina vitu hivyo angani.

Basi angalia, katika zodiaka, ilianza na kitu gani? Kitu cha kwanza katika zodiaka ni bikira. Kitu cha mwisho katika zodiaka ni Leo yule Simba: kuja kwa kwanza kwa Kristo kupitia kwa bikira; kuja kwa pili, Leo yule Simba, Simba wa Kabila la Yuda.

Ndipo Henoko akamaliza katika siku zake, ama kule nyuma katika hizo, lile piramidi. Na, bila shaka, hatuna wakati wa kuliwekea msingi na kuonyesha jinsi piramidi hilo lilivyokuja kupitia kwenye vile vyumba na kadhalika. Inazungumza moja kwa moja hata kwenye wakati wa mwisho sasa. Wao wako kwenye chumba cha mfalme sasa kwa vile vipimo. Bali jiwe la kichwani halikuwekwa kamwe kwenye lile piramidi. Na hiyo inakaa ikiwa kamilifu kabisa kiujenzi ama—ama kiuashi, mpaka hata we—wembe mdogo mwembamba… Nao hawajui jinsi wao walivyopata kulijenga, hawaelewi—jinsi wembe ungeweza kamwe kupita katika sehemu ambazo zingeungwa kwa chokaa, na hakuna chokaa ndani yake. Ni kamilifu tu, imewekwa pamoja.

Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo wakati Kristo na Kanisa wanapokuwa mmoja. Hakuna chokaa katikati; hakuna kilicho katikati, ni Mungu tu na huyo mtu— Mungu, Kristo, na huyo mtu.

Sasa, lakini lile jiwe la kichwani, wao hawajalipata bado. Mnajua lile Jiwe la Skonsi walilo nalo kule Uingereza la kutawazia wafalme—ama ku—kuwatia taji na kadhalika? Bali lile jiwe la kichwani…

Angalia kwenye noti ya dola ya Marekani; utaiona kwenye noti ya dala ya Marekani. Kwenye upande mmoja, upande wa kushoto, kuna Muhuri wa Marekani, tai aliyeshika mikuki. Kwenye upande wa pili . . . Hii inaitwa Muhuri ya Marekani. Bali kwenye upande wa pili kuna piramidi, na juu yake, jicho kuu. Halafu chini hapa inasema, "Ile Muhuri Kuu." Mbona iwe ni Muhuri Mkuu katika taifa hili, hata juu ya Muhuri ya taifa letu? Mnaona, haidhuru utafanya jambo gani, Mungu anaifanya inene jambo lile hata hivyo. Mnaona? Yeye humfanya mwenye dhambi kunena juu ya jambo hilo; Yeye huyafanya mataifa kunena juu ya jambo hilo; kila kitu hakina budi kuzungumza juu Yake, kama u—unataka kuamini jambo hilo ama hutaki. Liko papo hapo.

Sasa angalia, kuna jicho kwenye hiyo—jicho la Mungu. Na kwa sababu hicho kifuniko hakikutoka, ile Muhuri ya Kichwani, kwa sababu ilikataliwa, ambapo ilikuwa ni Mwana wa Mungu, Jiwe la Pembeni la hilo jengo, Muhuri ya Kichwani ya lile piramidi, na haya yote.

Sasa, sasa, mimi . . . Sitaki ku- . . . Wakati mwingine wao hunasa mambo haya, na yanatoka nje miongoni mwa ndugu makanisani—wa makanisa mengine. Nao wanapofanya jambo hilo, ndipo hao ndugu wakati mwingine wanapata mawazo mabaya, ya kwamba ninasema jambo fulani juu ya hao ndugu. Bali sisemi. Mimi . . . Kama mngalisikiliza tu na kufahamu (mnaona?), mimi sineni juu ya ndugu ye yote, maana jambo hilo halifai kwa hao ndugu kunena kuhusu—mmoja juu ya mwingine. Inatupasa kushuhudiana mazuri, si kusemana. Bali ninapozungumza wakati mwingine juu ya madhehebu fulani kama vile Presbiteri, Methodisti, ama kadhalika, wao wanasema, "Mnaona, anayapinga." Mimi simpingi ndugu aliyemo mle wala dada aliyemo mle. Utaratibu unaoutenganisha undugu ndio ninaonena dhidi yake. Watoto wa Mungu ni familia moja na si—si makundi mbalimbali.

Na baadhi yao wanasema, "Sitahusika nalo, kwa sababu hilo ni la Presbiteri nami ni Mmethodisti." Mnaona? Sasa, hilo silo . . . Mnaona, ni huo utaratibu wa madhehebu hayo unaovunja huo undugu. Mnaona? Sasa hilo . . .

Kama nilivyosema: Kama ulikuwa kwenye mto ukitelemka katika mashua inayoonekana bovu na ya kale na ulikuwa unaenda kujaribu kuvuka maporomoko, nami najua ya kwamba jambo hilo halitafanikiwa, vema basi, mimi sipigi makelele, kukukemea; ninajaribu kukutoa kwenye mashua hiyo (mnaona?); kwa maana mashua ndiyo itakayovunjika, nawe—nawe—nawe utaachwa umeketi peke yako majini. Kwa hiyo—kwa hiyo si—si yule ndugu katika ile mashua, bali ninampigia makelele yule ndugu kumwonyesha yale yatakayotukia.

Vema, taratibu hizi zote, ambazo wanadamu wameunda katika ufanisi wao, hazina budi kuvunjika. Hivyo tu. Lazima wafikie. . .Hatuna budi kufikia kwenye umoja, kwenye undugu. Hilo limekuwa . . .Kusudi la maisha yangu ni kujaribu kuunganisha wala si kuyavunja madhehebu, bali hebu wao waache mawazo yao na wawe ndugu kwa kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Wazo ndilo—ndilo hilo; hapo ndipo nimesimama.

Vema sasa, kama wandugu wangeangalia jambo hilo, mimi. . .Wengi wa ndugu zetu, hata kwenye safu zetu za Injili Yote, wao hawaamini ya kwamba Wabatisti, na Wamethodisti, na Waluteri, na hao wengine wana nafasi. Bali mimi. . .Sasa, huenda wanasema kweli, bali mimi sikubaliani na jambo hilo. Naamini ya kwamba ule wakati hapa, wa Wakati wa Waluteri, na wakati huu hapa ulioitwa, naamini, Wakati wa Sardi, halafu Wakati wa Filadelfia kwa ajili ya Wamethodisti, halafu Wapentekoste, Wakati wa Laodikia. . . Naamini hizo ni nyakati, naye Mungu katika kila mmoja wa nyakati hizo alichukua watu walioteuliwa. Na katika hilo, kama vile—Waebrania 11 isemavyo ya kwamba hao pasipo sisi hawakamilishwa. Mnaona? Lakini sasa, Kanisa limekuja kutoka kwenye hili, likija katika walio wachache wakati wote, hata limefikia katika Wakati wa Kipentekoste.

Sasa, sababu ya kusema jambo hili: ni kwamba mpate fununu juu ya kile yule dada alichoota. Nayo ndoto yake kweli inalingana na—na yale niliyokuwa nikifundisha.

Angalia, sasa hapa, sasa mambo haya yote ambayo I Petro aya ya 6 na ya 7 inawaambia, yaliyoletwa na imani yenu, hiyo ndiyo ya kwanza. Sasa, nasema ya kwamba watu wanadai kuwa na sifa hizi bila hata kuzaliwa mara ya pili. Nami naamini nilitoa tamshi la kijeuri na kusema ni kama ndege mweusi akijaribu kujibandika manyoya ya tausi na kujifanya tausi; hawezi kufanya jambo hilo. Yawapasa kuwa ni unyoya wa kawaida ulioota toka kwake. Mwili wake hauna budi kutoa unyoya huo.

Na daima—na daima nimeshtakiwa kuwa mkali kwa dada zetu juu ya kuwa na nywele zilizokatwa, na kujipodoa nyusoni mwao mwote, na kadhalika. Daima nimelaumiwa kuwa ni mkali kwa dada zetu. Si kwamba nina kitu dhidi ya jambo hilo. Sisemi mwanamke huyo si mwanamke mzuri, ya kwamba yeye ni ninii—kahaba wa mitaani ama cho chote kile. Hiyo siyo nia yangu. Bali hivi ndivyo ilivyo: wakati yeye anapoweka vitu chungu nzima vya bandia kwa nje, inaonyesha kuna ubandia mwingi mno humo ndani (mnaona?), mahali ambapo panapaswa kujazwa na Kristo. Kwa maana nje daima huonyesha kile kilicho ndani. "Kwa matunda yao mnawatambua." Mnaona? Na ambapo Kristo anapaswa kuwa humo ndani, na kushughulikia ninii—Mungu, na kushughulikia

mambo mengine, badala ya uzuri mwingi wa bandia, na—na, ninyi mwajua, kope za kijani, na yasiyoonekana kama ni ya kibinadamu, na takataka zote za namna hiyo. . .Mimi siyapendi mambo hayo; wala siamini Biblia inayakubali. Kwa hiyo mimi—mimi napenda tuwe tu jinsi tulivyo.

Angalia sasa, kama yeye hana kucha zo zote za vidole na anataka kuweka chache, iwapo hana meno yo yote na anahitaji machache, huna mkono na unataka mmoja, huna nywele nawe unataka nyingine, huna vitu hivi, hilo ni jambo lingine. Bali unapong'oa meno yako ya kweli na mazuri, kwa sababu ati si meupe kama yanavyopaswa kuwa, basi umefanya makosa. Kama una nywele nyekundu nawe unataka nyeusi, nawe unashuka unaenda hapa chini na kuzitia rangi nyeusi, kwa sababu tu. . .Umefanya makosa. Naam, nafikiri hivyo. Bali jambo muhimu. . .Hakuna Maandiko kwa ajili ya jambo hilo, ni kukata nywele zako tu, kuna Andiko juu ya jambo hilo, nina mengi ya hayo. Kwa hiyo basi, tunataka kuhakikisha kabisa ya kwamba jambo hilo ni kweli. Sasa.

Sasa, sasa, dada yetu katika kuota, aliota ya kwamba yeye. . .Vema kwanza, alifadhaika: "Kuna haja gani ya kuendelea na kujaribu kujitahidi katika maisha kama Mungu anatutaka tumpokee Roho Mtakatifu nasi hatuna Huyo?"

Sasa, sidhani. . .Huenda wao wananasa huu, bali kama hawaunasi—kama wanaunasa, ni kwa ajili ya kanisa peke yake. Mnaona? Sasa, na iwapo ndugu fulani ataupata huu, nawe usikie sauti yangu, ndugu, juu ya jambo hili, kumbuka, ninafundisha tu kanisa langu. Wewe daima, mbele ya kusanyiko lako. . .Chunguza hizo—hizo kanda, na endapo hutaki kusanyiko lako lizisikilize, usiwaruhusu wazisikilize. Bali mimi—mimi ninajaribu tu kuliambia kundi hili dogo hapa ya kwamba mimi—ambalo mimi na Ndugu Neville, kwa Roho Mtakatifu, tunajaribu ku—kuwachunga na kuwafundisha. . .

Sasa, kuna baadhi ya mambo haya ambayo huenda mkayapinga vikali. Kwa hiyo kama yapo, kama tu nilivyosema daima juu ya kula kuku aliyekaangwa: Unapofikia kwenye mfupa humtupilii mbali huku, unatupa tu mfupa. Kwa hiyo fanya hivyo daima. Ukila sambusa ya tunda jekundu na ukute punje, hutaitupa hiyo sambusa, utatupa tu hiyo punje. Kwa hiyo fanya jambo lilo hilo katika kuusikiliza huu.

Sasa, na—naamini ya kwamba—ya kwamba sa—sababu ya kuwa na kuchanganyikiwa kwingi leo juu ya Roho Mtakatifu, Hilo halijafundishwa sawasawa. Ninaamini ya kwamba ubatizo unafundishwa, na kusema tu, "ubatizo," lakini basi uwe. . .Kama vile ukisema, "motokaa." Lakini sasa, nina mafundi wengi wa magari katika kanisa hili, nami sijui cho chote juu yake, kwa hiyo kama nikifanya kosa, ndugu, mimi. . .Kumbukeni mimi si fundi wa magari.

Hapana budi kuwe na koili, na plagi, na pointi, na vilango, na kila kitu kinginecho kinachoifanya motokaa. Na unapozungumzia kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuna mambo mengi yanayoambatana na huo. Mnaona? Kuna mengi yanayoambatana na huo. Na jambo hili ndilo linalonifanya nifikiri ya kwamba Mungu anathibitisha Roho Mtakatifu yuko hapa. Mnaona?

Basi, Petro alisema kwanza, imani. Sasa angalia jambo hilo kwa makini sana sasa. Tutafundisha jambo hili kwa dakika chache. Imani, sasa, ndiyo ya kwanza kwako. Tia katika imani yako, nguvu; katika nguvu zako, maarifa; katika maarifa yako, kiasi; katika kiasi chako, saburi; katika saburi yako, utauwa; katika utauwa wako, upendano wa ndugu, fadhili za kindugu, halafu upendo. Na mtu ye yote anajua ya kwamba upendo ni Mungu. Mungu ni upendo. Mnaona?

Sasa kwa kuwa—halafu kutoka katika jambo hili, halafu kuleta jambo hili kwenye zile Nyakati Saba za Kanisa, Mungu anajenga katika nyakati saba za kanisa Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo. Kupitia kwenye wakati wa Filadelfia, wa Thiatira, wa Pargamo, na wa Smirna, Efeso, wakati wa kanisa ambao Yesu alisema, "Kama—kama Bwana Arusi akija katika zamu ya kwanza ama zamu ya saba, wanawali hawa wote waliamka." Wao walikuwa—wao waliamka, wanawali wa Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, na Laodikia. Umeona hilo? Ilikuwa ni wakati wa saba ambapo alikuja na kuwaamsha hao wanawali waliolala. Jambo hilo linawaleta kutoka kote kote huko nyuma mpaka hapa (mnaona?), kwa kuwa katika jambo hili, kupitia katika miaka, nyakati, Yeye amejenga Bibi-arusi, akamzaa Bibi-arusi, akamzaa Bibi-arusi duniani kwa ajili ya Kristo. Na kwa njia ile ile anayomzaa Bibi-arusi huyu, amewazaa watu binafsi.

Sasa, ninawekea jambo hili msingi, ili kwamba mwone wakati ile ndoto ya dada inaposimuliwa.

Sasa, mambo haya hapa hasa hayana budi kuwa ndani ya Mkristo daima kabla Roho Mtakatifu hajawatia muhuri kabla hiki hakijaja upande wa juu na kufanya kitu kimoja kikamilifu.

Sasa, ndoto ya dada yetu sasa. Yeye alipata wasiwasi kama ana Roho Mtakatifu ama hana. Wakati alipolala kwenye Kitanda cha watu wawili, ambapo mumewe alikuwa anasoma gazeti (na ana watoto, kama nilivyo nao mimi, nao daima wanafanya makelele na kadhalika), na kwa hiyo katika jambo hili, alilala usingizi kwa kama dakika kumi ama kumi na tano; ndipo akaota. Naye kamwe asingeweza kuielewa wala kuikumbuka tangu mwaka mmoja uliopita, karibu, mpaka ujumbe huu ulipofundishwa. Ndipo wakati nilipokuwa ninaufundisha, yote ikamrudia.

Naye aliota ya kwamba alikuwa anaomba. Alikuwa anatembea sakafuni kwanza, kabla hajaota ndoto, na kusokota mikono yake, na kuwaza, “Bwana, hivi mimi nina Roho Mtakatifu? Unaweza kunithibitishia. Wengine wanasema ati—ati kwa sababu nilipiga makelele, ama wengine walisema ati kwa sababu nilinena kwa lugha. (Nasi tunaamini katika hayo yote.) Lakini hivi kweli mimi ninaye?”

Ninaamini katika mambo hayo yote, sifa hizo: kunena kwa lugha, na kupiga makelele, na kila namna ya madhihirisho. Ninaamini katika kila moja ya hayo. Bali kama yako bila *hili*, kuna kasoro. Unaona? Sasa, mnaona? Wewe...Unaona, una ganda.

Angalia, naye alikuwa amefadhaishwa na jambo hilo, kwa hiyo alilala tu chini kukingama kwenye kile Kitanda cha watu wawili, ambapo mumewe alikuwa anasoma, ndipo akaingia usingizini. Basi akaota alikuwa juu ya mlima fulani. Na katika mlima huu...Ninii bora sana...Sina ile karatasi mbele yangu, bali nafikiri ni namna hii: Yeye aliota ya kwamba aliona ki—kitu kama sanduku la mwamba, kama jukwaa limewekwa moja kwa moja juu ya mlima huu. Naye bwana wake alikuwa nyuma yake. Ndipo akaona mtu mkubwa amesimama pale amevalia nguo za kazi, mikono ya lile vazi imekunjwa, akiteka maji safi sana aliyowahi kuona na kuyamwaga kwenye sanduku hili, sanduku hili la mwamba lililokuwa juu ya ule mlima. Nalo sanduku hilo la mwamba halikuweza kushikilia hayo maji; nayo yalitiririka yakatoka mle na kuchemsha taka zote na vijiti na kila kitu mle ndani, na kuvichemsha, kisha yakatiririka mlimani. Nayo yakatiririkia kwenye miguu yake, naye alikuwa amesimama katikati ya taka hizo; ila tu hazikumchafua. Ndipo—ndipo basi akauliza kwa nini lile sanduku halikuyazuilia, ndipo yule mtu akasema, “Hayo si maji. Huyo ni Roho Mtakatifu,” na akasema; “hakuna kitu kinachoweza kumzuilia Huyo.”

Kisha kasema, “Ndipo akarudi akachukua ndoo nyingine kubwa—nayo ilikuwa imejaa asali—halafu akaimwaga ile asali mle na kusema, ‘Sasa, itaizuilia hii.’” Naye alifikiri ya kwamba lile sanduku lilikuwa—lile sanduku la mwamba lingepasuka na kuimwaga ile asali, bali halikupasuka. Hatimaye ilishikamana na likaizuilia.

Akageuka akashuka mlimani. Alipokuwa anashuka mlimani, alisimama chini ya ule mlima na kuangalia nyuma. Akaona vijito vitano vya maji haya masafi kabisa, yasiyochafuliwa na vitu ambavyo yalikuwa yamevipitia, yangali mazuri na masafi, yakija mbio. Kisha yakapunguza mwendo; halafu karibu kutoweka. Naye alikuwa akishangaa kama yatawahi kufika chini ya ule mlima—vijito vitano—ndipo akaamka. Nafikiri hiyo ni karibu na kuwa sawa, sivyo, Dada Shepherd?

Sasa, mara nilipoichukua ile barua na kuifungua, kabla sijaisoma, nikaona ile ndoto yake. Sasa, hivyo ndivyo ndoto zinavyofasiriwa. Sasa, wengi wenu mmenijia na ndoto na—na kuniambia mambo juu ya ndoto. Ninasema, "Ngoja kidogo. Hukuisimulia yote" (mnaona?); nami narudi nyuma na kuichukua. Basi kama huwezi kusimulia ulivyoota, unajuaje fasiri hiyo ni kweli ama si kweli? Mnaona? Huna budi kuwa na—huna budi kuiona hiyo ndoto. Ono halina budi kuonyesha hiyo ndoto. Basi unapoiona hiyo ndoto ambayo huyo mtu aliota, nawe ungeweza kuwaambia kabla hawajakwambia, basi unajua hiyo fasiri . . .

Vema, naamini hiyo iko katika Maandiko pia. Danieli wakati mmoja (hiyo si ilikuwa ni kweli?) alisema . . . Naam, naamini . . . Imetukia kwamba nimewazia juu ya jambo hilo basi. Mnaona? Bali daima unaona hiyo ndoto, sasa, iwapo hiyo tafsiri ni kweli. Mtu fulani akianza kukusimulia ndoto, unawakatiza tu, unasema, "Ngoja kidogo. Na ilikuwa *fulani*, pamoja na *fulani*, kuongeza *fulani*."

Kisha unasema, "Hiyo ni kweli kabisa." Unaona?

Mtu fulani, juzijuzi, alikuwa anajaribu kunisimulia ndoto aliyoota. Akasema, "Vema," akasema . . .

Nikasema, "Sasa, ndugu, mbona uliacha ile sehemu nyingine?"

Akasema, "Sehemu nyingine gani?"

Nikasema, "Uliota ya kwamba ulitupa jiwe hewani, nami nikalipiga risasi na vingine vikaingia kwenye jicho langu."

Akasema, "Hiyo ni kweli kabisa, Ndugu Branham."

Nao walichukua ile sehemu yake ya mwisho jana. Kwa hiyo ndiyo hivyo. Mnaona? Mnaona? Mbona huachilii . . . Wewe sema kweli juu ya jambo hilo. Lakini, mnaona, daima inafunua kile—inakuambia ndoto yako, kile ulichoota. Ndipo unajua ni kweli.

Naam, hii hapa fasiri ya ndoto yake. Yeye alisumbuka juu ya Roho Mtakatifu. Naam, kwa vile aliona lile sanduku juu ya ule mlima lilikuwa la mwamba, *sanduku la mwamba* ni "kukiri kwa mwamba." Sasa, kama vile Yesu alivyosema katika Maandiko, Yeye alisema . . . Petro alisema . . . Yesu alisema, "Watu hunena Mimi, Mwana wa Adamu, kuwa ni nani?"

Mmoja alisema, "Wewe ndiwe Eliya, na Musa, na kadhalika."

Basi Yeye akasema, "Lakini nanyi mwaninena ya kuwa Mimi ni nani?"

Akasema, "Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliye Hai."

Sasa, watu wengine husema…Sasa, kanisa Katoliki husema, Kanisa Katoliki la Kirumi linasema ya kwamba ninii Yake—kile ule mwamba ulikuwa ndicho ambacho Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu wala milango ya kuzimu haitalishinda Hilo,"… Wao walisema ulikuwa ni juu ya Petro, na Petro alikuwa huo mwamba, kwa maana *Petro* linamaanisha "jiwe dogo." "Na juu ya *jiwe* hili *dogo* nitalijenga Kanisa Langu." Na juu ya Petro wao—uhalifa wa kimitume—wao walilijenga kanisa.

Halafu kanisa la Kiprotestanti linasema, "Hilo ni kosa," ya kwamba alilijenga Kanisa juu Yake Mwenyewe.

Sasa, si kuwa asiyekubaliana, bali mimi—nionavyo mimi, wote wamekosea, kwa maana Yeye hakulijenga kamwe juu ya Petro, wala hakulijenga juu ya nafsi Yake; bali ni juu ya ufunuo wa Petro kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Mnaona? "Watu hunena kwamba Mimi, Mwana wa Adamu…"

"Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliye Hai."

"Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona: mwili na damu havikukufunulia hili (seminari fulani. Mnaona?); bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Wewe ndiwe Petro, juu ya mwamba huu (wa kukiri, juu ya ufunuo huu) nitalijenga Kanisa Langu."

Na hiyo imekuwa…Kila wakati wa kanisa umekuwa na kuungama huko kwa mwamba mpaka kwenye mwamba huu wa kuungama wa Laodikia. Na sasa, huwezi kufanya kanisa takatifu. Hakuna kitu kama kanisa takatifu wala madhehebu matakatifu. Roho Mtakatifu anaweza kuhubiriwa ndani yake, bali mle ndani unakuta wazuri na wabaya, wapotovu, wasiojali, na cho chote kile. Kwa hiyo madhehebu hayatabeba… Huwezi kusema, "Tunaye; hakuna wengine walio Naye." La, bwana! Roho Mtakatifu humiminwa juu ya watu binafsi. Ni mtu binafsi.

Kwa hiyo basi, ule mwamba…Kanisa hili la Pentekoste la siku za baadaye, ambalo limempokea Roho Mtakatifu waliyempokea hapo awali… Kote kote katika nyakati, wao walimpokea Roho Mtakatifu, bali si kwa kipimo walicho Naye sasa; maana ni kurudishwa kwa ule wa kwanza. Tunapochukua kinara cha taa, Alfa na Omega, jinsi walivyouwasha ule mshumaa wa kwanza: ulizidi kupanda na kupanda juu, kisha ukazidi kufifia, halafu ukarudi tena (mnaona?), wa kwanza na wa mwisho na kadhalika.

Sasa, bali katika wakati huu wa kanisa Ujumbe unamwagwa katika kanisa. Bali mwili wa kanisa, wenyewe, kwa jumla…Kama vile—maskani hii, tutasema; hapo ndipo

yeye anapokuja kanisani kuabudu. Maskani hii si maskani ya Roho Mtakatifu. Hakuna kitu kama hicho. Watu binafsi wanaohudhuria kanisa hili ndio maskani ya Roho Mtakatifu. Hao ndio maskani iliyo na Roho Mtakatifu, bali si kanisa katika jamii ya kundi. Kwa hiyo Huyo anamwagika.

Lakini basi, mtu huyu aliyekuwa anamimina yale maji, yule mjumbe kwa kanisa, akiumwaga Ujumbe kanisani. . . . Bali yale maji yalikuwa yanafanya nini? Yalikuwa yakichemsha taka zote zilizokuwa ndani yake. Hicho ndicho Roho Mtakatifu anachofanya: anazichemsha.

Sasa, sasa, asali iliwakilisha upendano wa ndugu, fadhili za kindugu, ambao ni wakati huu. Ndiyo kwanza nimalize kuwaambia (mnaona?) juu ya fadhili za kindugu, wakati tunaoishi sasa.

Sasa, unaweza kusema, "Angalia, hakika si—si—simpendi Ndugu Neville," ama, "Kweli simpendi Ndugu Jones; simpendi Ndugu *Fulani*," na kitu kama hicho. Bali acha kitu fulani kimpate; ndugu, moyo wako unavunjika. Jambo hilo nusura likuue. Unaona? Tunaweza kupata fadhili za kindugu na kuhurumiana. Mnaona? Bali kuzidumisha katika kundi la watu. . .

Mbona unamjali ndugu huyo? Kwa sababu ulimega mkate pamoja naye hapa madhabahuni, kama utakavyofanya usiku wa leo; unashiriki pamoja naye; ulimpa mkono; unaabudu pamoja naye. Yeye ni ndugu yako. Naye anaweza kufanya jambo fulani katika mwili ambalo usingekubaliana nalo, kwa sababu kwa namna fulani unakaa (jambo ambalo halikupasi kufanya lakini)—unajiepusha naye kidogo. Lakini katika kilindi cha moyo wako, kama kitu fulani kingelimpata huyo ndugu, nusura kingekuua, ama dada huyo.

Mimi—mimi ni mzee. Wakati mmoja nilikuwa kijana lakini sasa ni mzee. Nimeona jambo hilo likitukia kila wakati. Kuwasikia watu wakisema, "Vema, sitajishughulisha tu naye tena." Na jambo fulani linampata mtu huyo, nusura limwue; anawaza, "Ee, Mungu, nimemwacha ndugu yangu mpendwa aondoke bila kupatana naye (unaona?) tena." Unaona? Unaona, ni upendano wa ndugu. Unaonekana kama hutanata, bali unanata. Asali, inanata.

Sasa, kwa kuwa alitoka kule, akashuka kwenye kile kilima akaenda chini ya kilima. . . Sasa, maji haya yenye utukufu yalikuwa yakibubujika kutoka juu ya kile kilima katika vijito vitano. Sasa, *tano* ni namba ya neema: J–e–s–u–s, I–m–a–n–i, N–e–e–m–a. Mnaona? *Tano* ni namba ya neema. Vijito vitano vilikuwa vikitiririka kutoka *hapa* juu kwenye kihori na kutiririkia kupitia *hapa*. Na kila mmoja wa nyakati hizi ulikuwa na huo mwamba wa kuungama. Watakatifu wanalala, wanaendelea kungoja, kungoja, kungoja, kungoja (mnaona?) na

kuendelea hata kwenye wakati huu, bali hivi karibuni Roho Mtakatifu, akimwagwa kutoka kwa Kristo, atakuja na atalitia Kanisa muhuri, kisha Kanisa litanyakuliwa. Litakuwa kitu kimoja kikamilifu cha Mungu, Bibi-arusi wa Kristo, atakayekuwa kichwa cha mambo yote. Mnanifuata sasa?

Sasa, alikuwa akishangaa...Sasa, katika ndoto yake alikuwa anashangaa, je! kijito hiki kidogo, kijito hiki kidogo kitawahi kufika kule chini. Mnaona? Kilikuwa kinakauka. Sasa, kwa kuwa yeye mwenyewe... Sasa hapa ndipo ninapotaka mfikie sasa. Yeye mwenyewe alikuwa anashangaa juu ya nafsi yake. Je! alikuwa na Roho Mtakatifu?

Sasa, nilijiepusha na kusema jambo hili siku chache zilizopita, nikifikiria ya kwamba kanisa lingekuwa la kiroho vya kutosha kulipata (na labda yanipasa kufunga kinasasauti hiki sasa hivi, lakini—kwa sababu sitaki itoke iende miongoni mwa ndugu); bali ungaliweza kunena kwa lugha, ungaliweza kupaza sauti, ungaliweza kucheza, ungaliweza kutoa pepo, kufanya lo lote utakalo, na bado usiwe na Roho Mtakatifu.

Je! hao wanafunzi hawakuja wakifurahi na kupiga makelele, kwa sababu pepo walikuwa wanawatii? Naye Yesu...Moja kwa moja miongoni mwao alikuweko Yuda? Je! Yesu hakusema katika siku hiyo alipokuja, ya kwamba "Wengi watakuja Kwangu na kusema, 'Bwana, mimi sikutoa pepo na katika Jina Lako nikafanya kazi kubwa,' Nami nitasema, 'Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, sikuwajua mimi.'" Mambo hayo si dalili ya Roho Mtakatifu. Kwa matunda yao mtawatambua.

Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, hivi sisi—inatupasa kunena kwa lugha?" Kweli, hizo ni karama za Mungu. Bali karama hizo za Mungu, bila ya sifa hizi ndani yake, hufanya jiwe la kujikwaa kwa asiyeamini. Mungu hakubali jambo hilo. Hizi hazina budi kutangulia. Na unapokuwa na imani, nguvu, maarifa, kiasi, saburi, utauwa, na upendano wa ndugu, ndipo Roho Mtakatifu anashuka na kukutia muhuri kama kitu kimoja, sawasawa na anavyozitia muhuri nyakati za kanisa kama kitu kimoja. Jinsi anavyomfanya Bibi-arusi Wake ndivyo anavyomfanya mtu Wake binafsi: anafanywa kwa vitu vile vile, kama vile Hawa alivyofanywa kutokana na Adamu, ubavu kutoka ubavuni. Hivi hapa vitu ambavyo huna budi kuwa navyo kwanza. Huwezi kujifanya unazo; huwezi kuviigiza; havina budi kuwa vimetumwa na Mungu na kuzaliwa na Mungu. Kuigiza kunasababisha tu kuchanganyikiwa.

Ni kama nilivyosema: Ungeweza kuwazia kumwona kipanga, akiketi pale na unyoya wa hua umechomekwa kwenye mabawa yake, aseme, "Mnaona, mimi ni hua." Yeye si hua, yeye ni kipanga, koho.

Ungeweza kuwazia ndege mweusi akiwa na manyoya ya tausi kwenye mabawa yake na kusema, "Unaona. . .?" Hicho ni kitu alichokichomeka mle ndani. Bali haina budi kutoka ndani ije nje, na izae Ukristo. Mungu, kwa nguvu za Roho Mtakatifu. . .

Dada yetu alikuwa amelowa miguu alipofika kule chini. Sisi sote tunamjua Dada Shepherd kuwa mwenye fadhili. . . Nyumba yake imefunguliwa. Yeye na Ndugu—sijali kama ni mzururaji, mwombaji, ama ye yote yule, wao watamlisha, wafanye lo lote wawezalo kumsaidia. Loo, Mungu alikubali jambo hilo, sehemu yake ya msingi. Na hapa kuna. . .

Sasa, shika somo hili: Hili hapa kosa la—la. . .(Sipaswi kufungulia kwa ajili ya jambo hili.) Kosa la Maskani ya Branham ndilo hili. Mnaona? Kuna namna mbili za imani; kuna namna mbili za nguvu, kama nilivyosema juzijuzi; aina mbili mbalimbali za maarifa; aina mbili mbalimbali za kiasi. Mmoja anafikiri ni kukatazwa. Wao wana. . .Hicho sicho kiasi ambacho Mungu anazungumzia habari zake. Ni hiyo hasira isiyo ya kitauwa na isiyozuilika uliyo nayo, na mambo ya upande huo, hamaki kali, kuzozana.

Saburi, na kadhalika, kuna mwigo wake, kujifanya, imani inayotokana na maumbile, nguvu zinazotokana na maumbile. Kuna kiasi kinachotokana na maumbile. Na mambo haya yote hutokana na maumbile.

Na sehemu kubwa sana ya imani yetu ni imani ya akili. Kwa kusikia Neno, sisi. . .kunatuleta kwenye kumtambua Mungu kiakili. Bali kama hii inatoka juu, loo ndugu, kama kamwe itaigusa *hii*, kuna imani ya kiungu, ya kiroho. Basi hiyo imani inafanya nini? Imani hiyo inatambua Neno peke yake. Haidhuru kitu kingine cho chote kinasema nini, inatambua Neno peke yake, kwa maana *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu.* (Naye Neno angali Mungu.) *Naye Neno alifanyika mwili,* akakaa *kwetu*. . . Na wakati Neno lenyewe linapomiminika katika imani yetu, imani yetu ya akili inakuwa ufunuo wa kiroho. . . "Na juu ya msingi huu nitalijenga Kanisa Langu," mnaona, si juu ya dhana ya akili ya kujiunga na kanisa, dhana ya akili ya jambo hilo, bali juu ya ufunuo. Wakati hivyo vijito vya neema vinamiminika ndani ya imani hiyo ya akili uliyo nayo, halafu juu ya huu, ufunuo wa kiroho, "Nitalijenga Kanisa Langu na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda." Mnaona? Hiyo inaonyesha italipinga, bali haitashinda. Loo, ni jambo tukufu jinsi gani.

Sasa, mnaona, imani, mito hii mitano. . . Nilikuwa na kipande cha choki hapa, bali nafikiri hakukileta. Bali hivi vijito vitano mnavyoona vikishuka kupitia hapa vinaichanganya hii pamoja. Imekuwa ni Roho Mtakatifu

aliyelifanya kanisa la Efeso. Roho Mtakatifu ndiye aliyeliosha kanisa la Smirna. Roho Mtakatifu ndiye aliyelitoa kanisa la Pergamo na kanisa la Thiatira katika zile Nyakati za Giza. Roho Mtakatifu ndiye aliyemjenga Bibi-arusi huyo, yule Mteule ambaye ametoka kwenye taratibu zote za madhehebu kote kote katika nyakati namna hiyo. Na kuna Bibi-arusi wa Yesu Kristo aliyeteuliwa na kuchaguliwa tangu zamani, ambaye Roho Mtakatifu amemwita atoke, yule Mteule. Na imekuwa ni Roho Mtakatifu katika wakati huu, wakati ule, wakati ule, ule, ule, ule, ule, ule na kuendelea hata juu; Roho Mtakatifu.

Basi sasa, kama vile katika watu binafsi, wema huu na kadhalika vina—(maarifa na kiasi)—vinatiwa kwenye imani yetu, ndipo Jiwe la Kileleni linapokuja, Roho Mtakatifu anavishikamanisha pamoja. Huo ndio Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu ni haba sana leo.

Hebu nione hapa. Nina vifungu vilivyoandikwa hapa chini. Hebu tuone. Nilikuwa na picha iliyochorwa hapa ku—kwa ajili ya ndoto yake. Mnaona? Hamwezi kuiona kutoka huko.

Sasa, kikitoka kwa Roho Mtakatifu, ni nini kinachokuja? Ndipo atakupa imani ya kimbinguni, imani ya kiroho, hii hapa chini. Ndipo imani hiyo ya kiroho hutambua tu Neno peke yake. Haidhuru mtu mwingine ye yote anasema nini, hai—haifai kitu. Hiyo inajua Neno tu. Kama mtu fulani akisema, "Siku za miujiza zimepita," imani hiyo inajua Neno peke yake.

Mtu fulani anasema, "Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu." Imani hiyo inajua Neno peke yake. Hiyo ndiyo imani halisi ya kiroho. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Inajua tu Neno.

Halafu, hiyo ilikuwa namba moja. Namba moja, ikija kwako, imani yako ya akili, papa hapa, anakuja Roho Mtakatifu, akishuka na kuingia katika imani yako ya akili akiifanya ya kiroho. Ndipo hiyo imani ya kiroho hukubali Neno peke yake.

Sasa, na namba mbili—tatu: Ndipo utakuwa na ya kiroho, utakuwa—utampata Roho Mtakatifu, na atavitia muhuri vitu hivi vyote ndani yako, wakati Roho Mtakatifu anapoifunika hii. Kutoka kwenye imani yako hadi kwa Roho Mtakatifu anakutia muhuri ndani pamoja na Kristo; ndipo mnakuwa mmoja. Amina! (Ondoa kitu hiki mbele yangu. Ni kizito kwenye mikono yako.) Mnakuwa mmoja. Mnaona, wewe na Kristo mnaishi pamoja. "Katika siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Mnaona? Ndipo hicho ni kitu kimoja kilichotiwa muhuri cha Bwana Mungu. Sasa, halafu vinathibitishwa na kuwekwa. Hapo wakati huo unapowadia, wao wanakuwa wana na binti za Mungu waliothibitishwa.

Mnakumbuka katika Kitabu cha Mathayo, sura ya 17, aya ya kwanza hadi ya 5, Yesu kwenye ule Mlima wa Kugeuzwa? Mmenisikia mimi . . . *Msikieni Yeye*, huo ujumbe ambao ndiyo kwanza, hapa yapata mwaka mmoja uliopita, nikahubiri huo ukapendwa sana na watu, *Msikieni Yeye*. Kufanywa mwana mwenye mamlaka katika Waefeso 1:5 pia: "Mungu ametuchagua tangu zamani tufanywe wana wenye mamlaka."

Mnaona, familia . . . Mwana anapozaliwa kwake, ni mwana wakati huo. Bali huyo mwana alikuwa na waalimu wa kumlea. Na iwapo huyo mwana hakufanyika—hakufanyika mwana wa namna iliyo halisi, hakufanywa mrithi kamwe. Bali kama alikuwa mwana halisi, na mwana ambaye angemtii babaye, basi huyo mwana alifanywa mwana mwenye mamlaka ama akawekwa mahali pake. Anakuwa mrithi wa kile alichokuwa nacho babaye.

Na hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa akifanya kwenye Mlima wa Kugeuzwa. Wakati alipomchukua Mwanawe Mwenyewe, baada ya kuthibitishwa kuwa Mwana halisi (mnaona?), na alikuwa amestahimili majaribu yote, Yeye alimpandisha kwenye Mlima wa Kugeuzwa kisha akamtia uvuli.

Mnajua, katika Agano la Kale walimchukua mwana, wakamvalisha mavazi mazuri na ya kupendeza, kisha wakamweka mbele ya hadhara. Nao walikuwa na sherehe za kumweka mahali pake, ama tunaziita kufanywa mwana mwenye mamlaka. Katika Wagalatia pale, kwa namna fulani ninafikiri Paulo anakuita kufanywa wana wenye mamlaka.

Naam, kwa kumweka mwana . . . Wahudumu watafahamu, na wasomaji wa kiroho wa Biblia, ku—kumweka huyu mwana mahali pake. Kwa maneno mengine, huyo mwana alikuwa mwana alipozaliwa.

Hapo ndipo watu wetu wa Kipentekoste walifanya kosa lao. Kuzaliwa katika familia na Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli, lakini basi hatuna budi tuwe wana halisi, waliofunzwa na mwalimu afaaye. Mnaona?

Sasa, kama mtu huko nyuma katika nyakati za kale alimpenda mwanawe, naye alimtaka awe mwana halisi, alitafuta mwalimu mzuri sana aliyeweza kumpata, mwalimu mzuri kuliko wote; maana alitaka mwanawe akue awe kama babaye. Mnaona? Kwa hiyo akamchukua mwalimu afaaye.

Naam, kama mtu duniani angefikiria juu ya mwalimu aliye bora sana, na Mungu je! Baba yetu? Sasa, Yeye hakuwachukua maaskofu, na makadinali, na makasisi; Yeye alimchukua Roho Mtakatifu kuwa Mwalimu wetu. Naye Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu wetu. Naye yu—yuko Kanisani, Naye humpelekea Baba ujumbe.

Halafu, vipi kama baba—yule mwalimu alikuja akasema, “Vema, Baba. . .” Naam, Yeye hataenda na kuchukua namna fulani ya mwalimu ambaye anataka jani kavu kwenye kofia yake, mwajua, unyoya, kama tusemavyo; aseme, “Loo, kama nikimwambia Baba kitu fulani kuhusu. . .Maskini mvulana huyo ni mtukutu kwa vyo vyote, lakini kama mimi—kama nikimwambia Baba, huenda Baba akanipandisha cheo.” Huyo si mwalimu anayefaa. Mwalimu afaaye ni mwaminifu, husema kweli. Naye Roho Mtakatifu hunena kweli anapokuja mbele za Mungu, kwetu. Naam.

Kwa hiyo Yeye huja. Unafikiri nini? Yeye angekunja uso leo kusema, “Binti Zako wote wanakata nywele zao, Nawe uliwaambia wasifanye hivyo. Wanao wana mawazo ya kimadhehebu sana hata tu hawawezi kufahamiana, na hiyo ni. . . Nao wanachukua *hiki* badala ya *kile* na *hiki* badala ya *kile*.” Jinsi hana budi kukunja uso. Bali jinsi huyo Mwalimu angependa kuja na kusema, “Loo, jamani! Huyo mwana ni mwana halisi. Yeye ni kama Baba Yake kabisa.” Loo, jinsi angependa kusema jambo hilo. Mnaona?

Ndipo Baba anajaa fahari na kusema, “Huyu ni mwanangu.”

Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya hasa kwenye Mlima wa Kugeuzwa. Unatambua palitokea Musa na Eliya. Naye Petro, akiwa ameshtushwa sana, ya kimbinguni yalikuwa yamefanywa, kile. . .Petro ameshtuka; akasema, “Na tujenge vibanda vitatu: kimoja Chako, na kimoja cha Musa, na cha Eliya.”

Alipokuwa katika kusema, Mungu akamnyamazisha. Akasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ninayependezwa Naye. Msikieni Yeye.” Mnaona? Mungu alijiweka mwenyewe kule nyuma na, “Huyu ni Mwanangu.”

Musa aliwakilisha torati. Manabii waliwakilisha haki Yake. Tusingeweza kuishi kwa torati Yake. Tusingeweza kuishi kwa haki Yake. Siombi haki; nataka rehema, si haki. Mimi siwezi kuweka sheria Yake, wala siwezi kutimiza haki Yake; bali nahitaji rehema Yake. Naye Mungu alisema sheria na haki vimetimizwa katika Yeye. “Yeye ni Mwanangu mpendwa Wangu. Msikieni Yeye. Huyo Ndiye, huyo Ndiye Mwenyewe.”

Basi, katika Agano la Kale wakati huyo mwana alipofanywa mwana mwenye mamlaka ama kuwekwa mahali pake katika familia, jina lake lilifaa vile vile kwenye hundi kama la baba yake lilivyofaa. Naam, bwana! Hawakuwa na. . . Walikuwa na pete katika siku hizo, i—ishara, muhuri; nao wangeitemea mate [Ndugu Branham anafanya sauti ya kutema mate kisha anapiga mimbara kwa ngumi yake—Mh.], wanaitia.

Hiyo ilikuwa muhuri. Hiyo ilikuwa tu . . . Yeye alivaa pete ya babaye, muhuri ya—yake; na hiyo ilikuwa bora tu kama ya baba yake.

Basi, baada ya Yesu kuwa mtiifu, Yesu kwa Mungu, Mungu alimweka mahali Pake: "Huyu Ndiye."

Naam, wakati mshiriki amezaliwa na Roho Mtakatifu katika familia ya Mungu naye amethibitishwa kuwa na sifa hizi ndani yake, kwamba Mungu anaweza kuona nguvu, maarifa, kiasi, saburi, fadhili za kindugu, na utauwa ndani yake, basi Mungu humtia muhuri ama anamweka mahali pake. Basi hapo, hapo ndipo unapowaona wana na binti za Mungu.

Halafu Waefeso 4:30 inasema, *Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri* mpaka *siku ya ukombozi* wenu. Naam, baadhi yenu Wabatisti mnaotaka kwenda hata kwenye usalama wa milele, naam, kama mtafikia kiwango hicho, nitasimama pamoja nanyi kwamba ni usalama wa milele, kama mtafikia mahali hapo. Bali kusema tu, mtu ye yote anasema, "Nitaenda kujiunga na kanisa la Kibatisti"; "Mimi ni Mpresbiteri"; "Nina usalama wa milele"; hilo ni kosa. Maisha yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba huna. Mpaka HIZI ziwemo na Mungu amekufanya mwana na amekutia muhuri kwa Roho Mtakatifu ukaingia katika ufalme Wake . . . Basi hakuna kutoka ndani yake. Wewe ni salama milele." "Aminini—Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye ninyi nyote na sifa zenu za kitauwa mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi.

Ninaamini kuna Bibi-arusi aliyechaguliwa tangu zamani. Ninaamini Mungu alisema Yeye angekuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyazi. Ninaamini katika kuchaguliwa tangu zamani: ya kwamba Bibi-arusi amechaguliwa tangu zamani; Yeye hana budi kuwepo. Ninatumaini niko pamoja Naye. Hiyo ni . . . Mnaona? Niko pamoja Naye. Sasa, ni juu yangu kutimiza wokovu wangu na Mungu mpaka mambo haya yamekubaliwa na Mungu halafu yakatiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu. Huyo hapo Roho Mtakatifu. Hizo hapo kazi halisi za Mungu. Imetiwa muhuri hata siku ya ukombozi.

Hiyo ndiyo iliyokuwa ndoto yake. Nilifikiri ilikuwa nzuri.

Sasa, basi, wakati Hilo linapofanya hivyo, wakati Kanisa hilo litakapofikia mahali hapa, ama huyo mtu binafsi . . . Kanisa litakuwepo. Hebu niliseme vizuri sana kusudi mlipate: Kanisa limechaguliwa tangu zamani kuwepo. Nataka kuwa pamoja Nalo, bali njia pekee nitakayokuwa pamoja Nalo, ni kuwa sehemu Yake.

Ninakuwaje sehemu Yake? Kwa kuwa ndani Yake. Ninaingiaje ndani Yake? Kwa ubatizo, kwa Roho mmoja. I Wakorintho 12: "Kwa Roho Mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," Mwili mmoja, tumebatizwa ndani Yake.

Bali huwezi kuvishikamanisha vitu hivi vidogo, useme, “Nilinena kwa lugha. Nimempata Huyo.” Unatoka unaenda hapa nje, nawe una hasira, na unaapa, na kufanya yasiyofaa (mnaona?), huko ni kutia manyoya ya tausi kwenye—kwenye ndege mwenye milio. Mnaona? Huwezi kufanya jambo hilo. Maisha yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba sivyo ilivyo. Bali wakati vitu hivi vinafanya kazi ndani yako kwa njia ya Mungu, basi umetiwa muhuri. Ndipo basi hakuna kuiga kuhusu hilo. Wewe ni wewe tu. Hapo ndipo maono, kazi kamilifu za Roho Mtakatifu wa Mungu, kila kitu kinadhihirishwa. Kwa sababu gani? Wewe na Kristo mnakuwa mmoja (natumaini jambo hilo linaeleweka), wewe na Kristo mnakuwa mmoja.

Nilikuwa na kitu kingine nilichokuwa nimeandika hapa nilichotaka kuwazia. Anatuleta kwenye mahali pa Uzima, ndipo unakuwa—unakuwa na Uzima wa Milele.

Sasa, nina Kamusi ya Kiyunani hapa, *The Emphantic Diaglott*. Nilisoma juzijuzi juu ya neno fulani.

Naam, katika Yohana 14—ama Yohana 3:16, tunaona mahali pamoja panasema, “yuna Uzima wa kudumu daima”; mahali pengine panasema, “yuna Uzima wa Milele.” Bali katika—katika tafsiri ya Kiyunani, katika Kiebrania inasema, “Uzima usio na mwisho.” Katika neno la Kiyunani, yuna *A-i-n-i-o-a-n*. . . Karibu kama “aeon.” Aeon ni wakati ambao hauwezi. . . Ni hesabu isiyoweza kuhesabiwa. Imepita mamilioni, matrilioni, mabilioni. Bali huu ni *aionion* ya wakati: Uzima wa Milele. Na neno la Kiingereza kwalo ni *milele dawamu*. Tunalijua kama milele, *Aionion* ama Uzima usio na mwisho. Mnaona?

Na iwapo una Uzima usio na mwisho, unawezaje kuangamia? Umekuwa sehemu ya Milele, na kuna kitu kimoja tu cha milele. Shetani si wa milele. La! Yeye—yeye alifanyika Shetani. Kuzimu si kwa milele. Kuzimu kuliumbwa; si kwa milele. Na miili hii si ya milele; iliumbwa. Bali Roho wa Mungu ni wa Milele. Hakuwa na mwanzo, wala hana mwisho. Na njia pekee tunayoweza kuwa na Uzima wa Milele (kutokana na neno hilo la Kiyunani *Zoe*, ambalo maana yake ni “uzima wa Mungu Mwenyewe”), tuna—tunakuwa sehemu ya Mungu tunapokuwa wana na binti za Mungu nasi tuna Uzima wa *Aionion*. Kwa hiyo sehemu inayoishi, sisi, ambayo inatambua Neno hili kutoka *hapa* mpaka *pale*, inayotambua, ni Uzima wa *Aionion*, Uzima usio na mwisho. Ni Uzima wa Mungu Mwenyewe ndani yetu. Amina. Whiu.

Juzijuzi, kwenye safari, nilikuwa na mazungumzo; Shahidi wa Yehova. Sasa, si kutoijali imani ya mtu ye yote. Tuna waongofu wengi sana wanaoketi hapa kutoka kwa Shahidi wa Yehova. Mmoja wa wadhamini wetu wa kanisa ni Shahidi wa

Yehova—alikuwa, kisha akaokoka, yeye na jamaa yake. Baba yake alikuwa msomaji, Ndugu Wooods na hao wengine. Ndugu zake wote na dada zake sasa, karibu wote wameingia na kumpokea Roho Mtakatifu, kwa sababu ya maono ya Mungu yakiwaambia yale waliyofanya na yale wao. . .Mnaona? Hilo lilisababisha jambo hilo.

Sasa, bali hapa Shahidi wa Yehova katika kitabu chao, kinasema ya kwamba pumzi unayovuta ndiyo nafsi. Sasa, hiyo haiwezi kuwa sahihi. Pumzi unayovuta siyo nafsi. Kama ndiyo, wewe ni—wewe ni nii. . .Wakati mmoja wewe ni nafsi ya namna fulani; wakati mwingine wewe ni ninii. . .Mtu mwingine amevuta nafsi hiyo. Angalia mahali ungalikuwa. Sasa, ile pumzi ni upepo, nao upepo ndio unaovuta ndani ya tundu la pua yako.

Sasa, wao wanachukua Andiko kutoka kule nyuma, "Kisha Mungu akapulizia pumzi ya uhai katika pua yake, naye akawa nafsi iliyo hai." Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Kama alikuwa mtu, alikuwa akipuliza pumzi ya namna gani kabla Mungu hajampulizia ndani mwake pumzi hii ya uhai? Mnaona? Ni pumzi ya namna gani. . .Yeye alikuwa mtu anayepumua, mtu anayeishi. Vema basi, kama hivyo ndivyo ilivyo, basi kila mnyama ni nafsi iliyo hai, maana wao wanavuta nafsi ya binadamu, na nafsi yetu, na vyote pamoja. Basi isingalimpasa Yesu kufa; kafara ya mnyama ingalikuwa imetosha. Mnaona? Kwa hiyo, ndugu, hiyo hoja haiji.

Lakini alivyofanya Mungu, Yeye alimpulizia pumzi ya Uzima wa Milele (Amina!), ndipo akawa nafsi iliyo hai, nafsi isiyoweza kufa. Sasa angalia sasa. Tutaingia kwenye asali moja kwa moja hadi kwenye viko vya mikono yenu. Angalia, akampulizia pumzi ya Uzima wa Milele puani mwake. Naye akawa nafsi ya milele, maana Mungu alipulizia (si kile maumbile yalifanya, bali aliyofanya Mungu)— akapulizia pumzi ya uhai puani mwake, naye akawa nafsi iliyo hai.

Halafu unaniambia mimi, "Adamu alikufa, Ndugu Branham." Lakini kumbuka, kabla Adamu hajakufa alikuwa na mwana-kondoo aliyemkomboa. Haleluya! Wale aliowajua tangu zamani aliwaita. Alimchukua mwana-kondoo apate kuwakomboa.

Yeye alikuwa ni mfano. Adamu alianguka. Kisha mwana-kondoo akatolewa kwa ajili ya Adamu, kwa sababu tayari katika pua yake kumekuwa na pumzi ya Mungu wa Milele; naye akawa nafsi iliyo hai. Yeye alikuwa mwana wa Mungu. Si pumzi yake, kama lile neno la Kiafrika (sijui neno lake la Kiyunani ni lipi sasa hivi, lakini. . .)—neno la Kiafrika wao wanaiita *Amoyah*, ambalo maana yake ni "upepo, nguvu isiyoonekana." Wanyama wanavuta *Amoyah*. Wenye dhambi wanavuta *Amoyah*.

Basi kwa nini sisi imetupasa kujitahidi kupata Uzima wa Milele kama hiyo ndiyo nafsi ya milele iliyopuliziwa ndani yetu kwa pumzi. Kwa nini imetupasa kujitahidi kwa ajili ya Uzima wa Milele? Inapingana, ndugu. Mnaona? Ha—haiwezi kufanya hivyo kamwe. Bali Mungu hasa, juu ya Adamu, alipumua pumzi ya Uzima wa Milele, naye akawa mtu wa milele pamoja na Mungu. Alikuwa na nguvu kama Mungu: alikuwa mungu aliye mdogo. Alikuwa mungu wa dunia, si Mungu wa Mbinguni sasa, mungu wa dunia.

Na siku moja wana wa Mungu watakuwa miungu tena. Yesu alisema hivyo: "Je! haikuandikwa katika torati yenu, 'Ndinyi miungu'? Basi kama mnaweza kuwaita wale Yeye aliowaita miungu, ambao Mungu aliwazuru, mnawezaje kunihukumu Mimi, kusema, ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?" Mnaona? Naam, tunaingia kwenye kitu fulani chenye kilindi. Sasa, angalieni jambo hili tunapolifafanua.

Naam, hawa hapa. Yeye sasa ni mwana wa Mungu, bali anafanya kosa. Yeye anajua anafanya kosa. Sasa kumbuka, Adamu hakudanganywa. Biblia ilisema hivyo: ITimotheo 3: "Adamu hakudanganywa, bali mwanamke ali—alidanganywa, alikuwa makosani." Adamu alikwenda pamoja na Hawa, kwa maana alikuwa mkewe. Vivyo hivyo na Kristo, hakudanganywa na Shetani, bali aliingia katika mauti pamoja na Bibi-arusi. Yeye aliendа kuwa pamoja na Bibi-arusi, apate kulikomboa Kanisa.

Adamu alijua alikuwa amekosea, kwa hiyo alitoka tu akaenda pamoja na Hawa. Mnaona? Bali kulikuweko na mwana-kondoo aliyetolewa kwa ajili yao, kwamba walikombolewa. Na hawa wana-kondoo leo, ambao walijulikana tangu zamani na Mungu na Mungu amewaita, kuna Mkombozi. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu; na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Hiyo ni kweli?

Kwa hiyo kuna Mwana-Kondoo aliyetolewa tangu kuwekwa misingi ya dunia, ambapo majina yao yamewekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Mwana-Kondoo alitolewa kufanya njia ya neema kusudi kila mmoja wao apate kufufuliwa. Mwana-kondoo aliyetolewa, mwana-kondoo wa Adamu.

Sasa angalia, kama vile Adamu alivyokuwa na mwana-kondoo aliyetolewa. Sasa, ndivyo na Kanisa leo. Simaanishi ka—kanisa. Mnajua nini? Sisemi kwa kukufuru, wala sitaki limuudhi mtu ye yote. Mimi siko hapa kufanya jambo hilo, maana tayari nimejieleza mwenyewe; niko hapa kusaidia. Bali kile ninachojaribu kufanya. . .Mnajua nini? Kwa kweli makanisa haya si Makanisa. Kuna Kanisa moja tu. Haya ni maloji (mnaona?); ni maloji. Sina kitu. . .Ni sawa, lakini

na—nataka kuwathibitishia jambo hilo mnamo dakika chache, ya kwamba hayo ni maloji. Wewe ni mfuasi wa loji la Methodisti, loji la Wapresbiteri, ama loji la Wapentekoste, kulingana na jambo hilo, hiyo ni . . . Mnaona? Maloji! Mnaona? Hamwezi . . . Mnaona, makanisa kweli ni maloji ambamo watu walio na wazo lile lile wanachukuliwa pamoja. Bali Kanisa ni moja. Nawe huwezi kujiunga na Kanisa; unazaliwa ndani Yake. Na unapozaliwa ndani Yake, wewe ni mshiriki Wake.

Ni kama tu jamaa yangu. Nimekuwa katika jamaa ya Branham kwa miaka hamsini na mitatu; wao kamwe hawakuniomba nijiunge na hiyo jamaa. Kwa nini? Sina haja na kujiunga na hiyo jamaa. Nilizaliwa Mbranham. Nawe unazaliwa katika Kanisa. Sasa, haya mengine ni maloji. Uliwahi kuwazia jambo hilo? Naam, bwana!.

Siku moja nilikuwa ninakata nyasi, nami nilikuwa nikiwazia juu ya, vema, kanisa kuu takatifu la Katoliki, wanavyoliita. Nilikuwa nikiendelea namna hiyo, nikikata nyasi, na kitu fulani kikanisimamisha wima kabisa, kasema, "Usiliite hilo namna hiyo." Nami nikaangalia kila upande. Nikaanza kuendelea kukata nyasi, na kikanisimamisha tena, kasema, "Usiyaite namna hiyo." Kasema, "Hayo ni maloji kama mengine. Wao si Kanisa. Kuna Kanisa moja." Mnaona? Wao ni wafuasi wa loji, maana unaweza kujiunga na loji, bali huwezi kujiunga na lile Kanisa. Lile Kanisa, unazaliwa ndani Yake. Unakuwa mshiriki Wake kwa kuzaliwa upya, halafu mmoja wa ile jamaa, ndugu au dada ndani Yake.

Naam, hebu niwasomee kutoka kwenye *Emphatic Diaglott* hapa kitu fulani, kwenye Ufunuo 17:3, katika *Ufunuo wa Emphatic Diaglott* hapa, nanyi angalieni tu jambo hili, jinsi hili linavyosema na jinsi—jinsi linavyolingana vizuri na jambo hilo: Ufunuo 16–17. Vema! Sasa, hebu tusome hapa kwa muda kidogo tu. Sikilizeni jambo hili kwa makini sana. Ufunuo 17:3:

> Na mmoja wa hao Malaika saba wenye . . . vitasa saba akaja na kusema nami, . . . (*Ninawasomea kutoka kwenye kamusi.*) . . . *akiwa,* "Njoo, nitakuonyesha hukumu ya *kahaba* huyo mkuu, *aketiye* juu ya maji mengi; . . . (*Nasi sote tunajua huyo ni Vatican.*)

Hapa tuna *Our Sunday Visitor* kule ndani kutoka kwenye kanisa Katoliki, likituambia hiyo ni nini hasa. Mnaona? Na jibu hili kwake lilisema, "Lakini ngoja kidogo." Kasema, "Kumekuwako na majina ya kila namna," kasema, "ambayo yangefanya nambari 666."

Nikasema, "Lakini ngoja kidogo!"

Kasema, "Jina lako lingefanya mia sita, siti—"

Lakini nikasema, "Mimi siketi juu ya milima saba nikiutawala ulimwengu hata hivyo." Mnaona? Mnaona, hiyo ni kweli. Mnaona?

> "...kuonyesha...hukumu ya *yule kahaba* mkuu, aketiye juu ya maji mengi;... (*Maji, Ufunuo 17:15, ni wingi na umati wa watu. Mnaona*?) ambaye wafalme wa nchi *wamezini* naye, nao wakaao juu ya nchi *wamelevywa* kwa mvinyo ya—ya *uasherati* wake." ...(*Sasa angalia.*)

> Akaniongoza, katika Roho, hata jangwani;... (*Emphatic Diaglott sasa. Mnaona*?)...nikaona mwanamke *ameketi juu* ya mnyama aliyevikwa *nguo* nyekundu sana, amejaa majina ya makufuru,...

Naam, katika ile ya Mfalme James inasema,...*amejaa majina ya kukufuru*. (Hebu kidogo. Naam, nitalipata hapa muda kidogo tu. Ufunuo aya ya 3.) Vema, hii hapa. Vema, Ufunuo, nilimaanisha 17, si 7, 17. Sasa isikilizeni aya ya tatu:

> *Akanichukua katika Roho hata jangwani, nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina ya kukufuru,...*

Hivyo ndivyo Kiingereza kinasema, bali kiyunani asili kutoka kwenye *The Diaglott* kinasema hivi katika Ufunuo 17:3. Sasa sikilizeni.

> Akaniongoza, katika *yule* Roho, hata jangwani; nikaona mwanamke *ameketi juu ya* mnyama *mwekundu sana*, mwenye kujaa majina ya makufuru,...

Hiyo ni tofauti sana, kutoka kwenye "majina ya kukufuru" hata kwenye "majina ya makufuru." Ni nini?

Nasi—na sasa, yeye alikuwa mama wa makahaba. Sote tunajua jambo hilo. Sasa, ni nini? Haikubidi kuwa...Vema, hiyo ni kweli. Hilo lingechukua kanisa Katoliki la Kirumi, bali limejaa majina ya makufuru: Methodisti, Batisti, Presbiteri, Luteri, na yote, yanayojiita makanisa ya Mungu—majina ya makufuru. Tofauti kubwa kati ya "majina ya kukufuru" na "majina ya makufuru." Wanajiita wenyewe Kanisa la Mungu na kujianika wenyewe mbele ya ulimwengu, na karamu za kadi, na kunywa pombe na kufanya yasiyofaa, na supu za jioni, na cho chote kile, na upuuzi wa kila namna hata... Kuna Kanisa moja tu. Unazaliwa ndani Yake. Huingii mle, mpaka umesafishwa katika Damu ya Mwana-Kondoo na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

Ni tofauti jinsi gani kati ya "majina ya kukufuru" na "majina ya makufuru." Mnalipata? Nililipata hilo asubuhi ya leo nilipokuwa nikisoma hapa kule—niliposhuka. Kitu fulani kikaniambia tu, "Nenda katika chumba chako; chukua *The Diaglott*." La, ni utii tu, hivyo tu. Nikaingia, nikafungua Ufunuo 17. Nikawaza, "Kwa nini unanitaka nisome hili?" Nami nikaanza kusoma. Mara nilipolifikia hilo, "Hilo hapo." Nikachukua penseli nikaandika. Nikasema, "Hilo hapo."

Sasa, wao wanapiga makelele juu ya mimi kuyapinga madhehebu. Ni majina hayo ya makufuru yanayojiita Makanisa ya Mungu, na Makanisa ya Kristo, na makanisa ya Methodisti, na makanisa ya . . . Ni maloji, si makanisa. Kanisa moja, ambalo ni Kanisa la Bwana Yesu Kristo. Basi ni Lipi? Mwili wa kisiri wa Yesu Kristo ukitenda kazi duniani, uliofanywa kwa mfuasi wa yo yote ya makusanyiko haya, ambaye angekuwa mshiriki wa Mwili wa Kristo. Huna budi kuzaliwa ndani Yake; si kujiunga Nalo. Na ku—kujiunga Nalo ni majina ya makufuru.

Mwanamke huyu, mwanamke huyu, nguvu zake . . . Nanyi mnaona hivi sasa mahali watakapowapeleka watu wote walio na mawazo tofauti juu ya dini na kuwapeleka Alaska. Mmeona hayo. Imani zetu zote tofauti . . . Na kile—ni kitu gani? Lile Baraza, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na Katoliki ina shughuli zao kubwa zinazoendelea kule Vatican sasa, kule ambako wanajaribu . . . Na maaskofu hawa wote na kadhalika, wao wanajaribu kufikia mapatano kuupinga ukomunisti, ulimwengu ukiupinga ukomunisti na huku unaungana tu na Ukatoliki.

Na ni kama tu vile ilivyo leo: sisi hapa, kama nilivyosema, tuna- . . . Dhahabu . . . Karibu tumefilisika. Tunakopa, tunatumia fedha sasa katika kodi zitakazolipwa miaka kumi na minne tangu sasa. Hivyo ndivyo tulivyokwisha. Ni nani aliye na pesa za ulimwengu? Kanisa Katoliki. Zingekopeshwaje Marekani? Kuhifadhi makampuni haya ya tumbaku na wiski na kadhalika. Hakika wao watazikopa kutoka kwa . . . Watakapofanya hivyo, wao watauza haki yao ya mzaliwa wa kwanza moja kwa moja kwa kanisa Katoliki la Kirumi. Tutaungana. Tazama jambo hili lililo dhahiri vivyo hivyo, dhahiri kuliko kusoma gazeti; hili hapa. Mnaona?

Wao ni Wamethodisti, Batisti, Presbiteri, na kadhalika, wakijiita kanisa la Mungu. Katoliki, na upuuzi wote wa namna hiyo, ni nguvu za mnyama huyu mwenye kujaa majina ya makufuru. Ukijiita mwenyewe, "Mimi—mimi ni . . . "

Nilisema . . . Nilienda hospitalini hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikienda kumwombea mtu fulani. Nikasema, "Tuta- . . . "Ilikuwa ni mama yangu. Nikasema, "Tutamwombea Mama."

Ndipo huyo bibi akasema, "Fungeni pazia hiyo."

Nikasema, "Hivi wewe si ni Mkristo?"

Akasema, "Sisi ni Wamethodisti."

Nikasema, "Asante. Nilifikiri labda wewe ni muumini." Nami nikafunga pazia karibu nami basi. Mnaona? Kwa hiyo kama Wewe si Mkristo hilo ni jambo lingine (mnaona?), lakini "Sisi ni Wamethodisti." Hiyo ni kukufuru!

Yule mnyama, makanisa, yanayojiita makanisa, hayo si makanisa. Hebu nihakikishe jambo hilo liko kwenye kumbukumbu. Hayo si makanisa; ni maloji. Watu wanajiunga nayo, bali huwezi kujiunga na Kanisa la Mungu aliye Hai. Unazaliwa ndani Yake kwa Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na unapobatizwa na Roho Mtakatifu, sifa hizi zinatiwa muhuri ndani yako na Roho Mtakatifu; na kwa hiyo, "Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi." Hawezi. Haya basi. Loo, jamani! Tungeweza kuzungumza mchana kutwa, sivyo?

Kanisa ni Mwili wa kisiri wa Kristo, uliozaliwa kwa pumzi ya Mungu. Mlilifahamu jambo hilo? Kanisa la Mungu limezaliwa kwa pumzi ya Mungu. Mungu alipulizia kiroho, pumzi puani, mwa Adamu, akawa nafsi iliyo hai. Mlijua Wapentekoste, ama Kanisa la kweli la Kipentekoste limezaliwa kwa pumzi ya Mungu? Hebu niwasomeeni jambo fulani kwa muda kidogo tu, juu ya jambo hilo tu. Hebu nione kidogo tu. Yohana Mt., ninaamini, ninakoelekea, nasi tutaona kama kanisa la Mungu ndivyo lilivyo ama sivyo lilivyo. Yohana Mt. . . .Hebu tuone, naamini hiyo ni kwenye 16, 19, 20. Vema. Hapa, naamini tutalipata papa hapa. Vema. Hebu niwasomeeni mwone kama Kanisa limezaliwa kwa pumzi ya Mungu au la, kama Adamu alivyokuwa hapo mwanzo. Angalia.

> Na *ikawa jioni, siku ile ya kwanza ya juma, pale walipokuwapo wanafunzi, milango imefungwa kwa hofu ya Wayahudi*; Yesu akaja, *akasimama katikati* yao, *akawaambia, Amani iwe kwenu.*
>
> *Naye akiisha kusema hayo, akawaonyesha* mkono wake *na ubavu wake*. Waka—*Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana.*
>
> Naye Yesu—*Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi,. . . nami nawapeleka ninyi.*

Angalia! Baba aliyempeleka aliingia ndani Yake. Naye Yesu, anapomtuma mwanafunzi, Yeye huingia ndani yake, mtu yule yule aliyetumwa! . . .

> *Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia,* akasema, *Pokeeni Roho Mtakatifu*. . .(Kanisa lililozaliwa kwa pumzi ya Mungu.)

Wakati kimo hiki kimejifinyanga chenyewe pale katika ile hali, pumzi ya Mungu inapopuliziwa, wanampokea Roho Mtakatifu. Ndipo wewe ni mwana wa Mungu. Unaweza kujiunga na cho chote unachotaka, bali umezaliwa katika Ka—Kanisa la Mungu Aliye Hai, umezaliwa kwa pumzi ya Mungu. Mungu aliwapulizia akasema, "Pokeeni [Ndugu Branham anatoa sauti ya kupulizia—Mh.] Roho Mtakatifu." Loo, jamani, haya basi. Si "Njoo ukajiunge, andikisha jina lako pale," na pamoja na supu zenu za jioni na kila kitu

kinachoadamana nayo. Unajiunga na loji. Unaweza kujiunga na loji, Kimethodisti, loji la Kibatisti, loji la Kipresbiteri, loji la Kikatoliki, ama loji la Kipentekoste, kitu cho chote unachotaka kujiunga nacho, bali unajiunga na loji. Bali unapokuwa mwana wa Mungu, umezaliwa kwa pumzi ya Mungu. Amina! Afadhali tuliache papo hapo sasa. Vema.

Uzima wa Mungu pia umo ndani yenu. Yesu alisema (hebu kidogo)—Yesu alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni tawi." Sasa angalieni. Ugomvi wao na Yesu ulikuwa nini? Ugomvi wao na Yesu, kwa sababu Yeye alikuwa Mwanadamu akijifanya Mwenyewe Mungu. Yeye alikuwa Mungu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo. Mnaona? Naye aliwaambia, akasema, "Msiniangalie Mimi. Si Mimi; ni Baba Yangu, Naye anakaa ndani Yangu." Mnaona?

Sasa, wao walikuwa wakiangalia maskini mwili huo mdogo uliozaliwa na Mariamu. Mnaona? Huo haukuwa Mungu; huo ulikuwa ni Mwana wa Mungu, bali Mungu alikuwa katika mwili huo. Ilikuwa ni Mungu. Yeye alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu basi nihukumuni Mimi. Bali ni yupi kati yenu anayeweza kunihukumu Mimi kwa ajili ya dhambi (kutokuamini Neno)? Ni Neno gani Mungu amenena ambalo halijatimizwa ndani Yangu Mimi? (Dhambi ni kutokuamini.) Ni nani kati yenu ananishuhudia kwamba nina dhambi? (Dhambi ni kutokuamini.) Nionyesheni Mimi. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Bali kama nikifanya kazi za nanii Yangu. . .ingawa hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizitendazo kwa kuwa zinashuhudia." La sivyo, "Baba yumo ndani Yangu, akishuhudia kwa nafsi Yake," maana Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Mnalipata? Vema sasa, uhai ule ule ulio kwenye mzabibu uko pia kwenye tawi. Utajiungaje na huo? Huwezi.

Niliona mti fulani si muda mrefu uliopita katika bustani ya Ndugu Sharrit kule Arizona, ulikuwa na matunda tisa mbalimbali ya namna ya mchungwa ndani yake. Ilikuwa ni nini? Ulikuwa m—ulikuwa mti wa mchungwa, chungwa lenye kitovu, bali ulikuwa—ulikuwa na li—limau, chenza, kangaja, na balungi; ulikuwa na kila namna. Nami nikasimama, nikautazama mti huo, nami nikasema, "Ndugu Sharrit, unataka kuniambia ya kwamba mti huo ni mchungwa?"

Kasema, "Hakika."

Nami nikasema, "Vema vipi—imekuwaje?" Nikasema, "Ninaona balungi hapa, na chenza hapa, na kangaja hapa, na limau hapa, na matunda haya mengine yote. Yamekujaje?"

Akasema, "Vema, unaona, yamepandikizwa."

"Loo." Nikasema, "Vema, ninataka kukuuliza jambo fulani. Sasa, unachuma balungi hili na limau hili. Sasa, mwaka ujao utafanyaje? Utazaa basi chungwa kutoka kwake?"

"Loo, la!" Kasema, "Utazaa limau!"

"Loo." Nikasema, "Asante." Mnaona?

Huwezi kufanya jambo hilo. Huwezi kujiunga mle. Bali alisema kila wakati mti huo unapokuwa mwaka mmoja zaidi na unatoa tawi mpya, litazaa machungwa, kama huo mzabibu wenyewe ukizaa tawi.

Na jambo ambalo tumejaribu kufanya ni kuwa wafuasi waliojiunganisha Kwake, nasi tunaishi chini ya jina la Ukristo; kwa sababu sisi ni (kama ilivyo—katika msemo wa kawaida) —"Sisi ni tunda la namna ya mchungwa," kanisa la Kikristo. Bali wakati mzabibu wenyewe unapotoa tawi, litakuwa kama tawi la kwanza ulilozaa. Kama Mzabibu wa kwanza ulipotoa, wao waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, kama ukipata kuzaa lingine, utaandika Kitabu cha Mitume nyuma yake. Hiyo ni kweli.

Kwa hiyo unajiunga tu na maloji. Bali unapozaliwa kutokana na mzabibu. . . Una tunda; hiyo ni kweli. Una tunda, bali unafanya nini nalo? Una mfano wa utauwa na kukana Nguvu zake. Unakana ishara; unakana maajabu; unamkana Roho Mtakatifu. Unakana kunena kwa lugha; unakana maono; unakana unabii. Unakana kuponya, na hata hivyo unajiita jina fulani. Si ajabu Roho Mtakatifu alisema, "Nguvu za—makundi ya watu waliojaa majina ya makufuru (hakika!), wakijiita wenyewe Wakristo, wakiwa na mifano ya utauwa lakini wakikana Nguvu zake. Hao nao ujiepushe nao, kwa maana katika hao wamo wale wanaowachukua wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi."

Kila namna ya madhehebu, kanisa linalobeba mengi sana ya mambo ya shirika la namna *hii* na shirika la namna *ile*. Vipi kuhusu shirika la Yesu Kristo? Mnaona? Tuna mambo haya mengine yote, na tunalemeza kanisa. Sasa, haya basi.

Huwezi ukajiunga na Kanisa kamwe; unajiunga na loji. Wewe ni mfuasi wa loji, kundi la watu kama vile loji lilivyo. "Tunaamini *hivi*; tuna taratibu zetu, na tuna siri zetu na kadhalika." Unafanya jambo lile lile wakati—wakati unapojiunga na linalojiita kanisa, bali huwezi kujiunga na Kanisa. Wewe ulijiunga na loji la wafuasi bali si Kanisa, kwa kuwa unazaliwa katika Kanisa hilo. Na mzabibu wenyewe sasa. . .Ngoja kidogo. Angalia! Nami nitafunga baada ya kitambo kidogo.

Angalieni! Tafadhalini, si—sikumaanisha kusema jambo hilo. Angalieni. Kama Mungu alimuimarisha Bibi-arusi huyu na Roho huyo, basi jambo hilo liliimarisha huyo mtu binafsi na Roho huyo. Mnaona? Ndipo umezaliwa kuwa katika Ufalme huo, halafu Uhai ule ule uliokuwemo ndani ya Kanisa *hili* katika Kanisa *lile*, na *lile*, *lile*, *lile*, *lile*. Na Uhai ule ule uliokuwemo katika lile ganda, ule Mzabibu, Yesu, umo katika

mshirika aliyemzaa Yeye. Utukufu! “Kwa mambo yale yale niyafanyayo, kazi nizifanyazo, ninyi nanyi mtazifanya.” Huyo hapo mshiriki wa kweli wa Mwili wa Kristo; hakuna namna fulani ya jina lililobandikwa kwake. Kazi zenyewe za huyo mtu binafsi zinathibitisha anakotoka. Hayo hapo Maisha yanayoshuhudia yeye ni nini.

“Wewe ni—wewe ni...Ni mfuasi—wewe ni wa kundi gani?”

“Mwili wa Kristo!”

“Vema, ulijiunga Nao wapi?”

“Sikujiunga; nilizaliwa Mle.” Mnaona? “Nilizaliwa Mle.’

Huna lazima ya kumwambia. Wao wanajua kilichotukia. Wewe tu... “Unawezaje kuwasha mshumaa na kuufunika kwa pishi?” Yeye alisema. Mnaona? La, la!

Unapozaliwa kuwa katika Ufalme huo wa Mungu, basi Uzima, Uzima uliokuwemo katika Yesu... Ndipo unawapenda watu. Ndipo haikubidi kuwashawishi watu waje madhabahuni. Huna haja ya kumshawishi mtu fulani kuja kuomba pamoja na wale walioko madhabahuni. Vi—vi—vitu hivyo vinabubujika vyenyewe tu, kwa maana umetiwa muhuri ndani yako. Wewe ni kitu kizima cha Mungu. Umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

Sasa, mnajua maana ya Roho Mtakatifu? Haimaanishi niliruka juu na kupiga makelele, na nilipata hisi za ajabu. Hayo ni sawa. Nimeruka juu na kupiga makelele na nikawa na hisi za ajabu. Nilinena kwa lugha. Ninaamini Roho Mtakatifu hunena kwa lugha. Hakika! Nimefasiri. Naam, bwana! Ninaamini jambo hilo pia. Bali hilo silo. Hilo silo ninalozungumzia. Kunaweza kuwe na kuvuja hapa mahali fulani. Kunaweza kuwe na kuvuja hapa katika saburi yako. Hebu mtu fulani akupige kofi shavuni. Unaligeuza lile lingine? Lakini unasema, “Mnafiki mchafu yule.” Basi kuna kuvuja mahali fulani kumeanza. Afadhali tuachilie mbali jambo hilo. Vema. Lakini mnajua ninalomaanisha? Bali unapotiwa muhuri kuwa katika Mwili wa Kristo, basi umejazwa Roho, nawe ni mwana wa Mungu.

Loo, laiti ningalikuwa na kama dakika kumi kusoma kitu fulani hapa, lakini mimi... Mngenivumilia kwa dakika ziingine kumi? Ninataka kusoma jambo fulani. Kidogo tu sasa. Nita-...Kweli, maharagwe hayataungua; nitawahakikishia tu (mnaona?), kama tutasoma tu hili kwa dakika chache tu. Ni zuri sana hatuwezi kuliacha lipite. Nimepata mambo machache hapa yaliyoingia moyoni mwangu hivi punde ambayo ningetaka kusema. Hebu tufungue Yohana Mt. sura ya 3, inayozungumza juu ya Uzima wa Milele. Hebu tuone inavyosema juu ya swali hili la Uzima wa Milele pamoja na Uzima wa Mungu. Sasa, sasa angalieni hapa.

*Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi.*

*Huyo* basi *alimjia* Yesu *usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu*;. . . *hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi*. . . *isipokuwa Mungu yu pamoja naye*.

Sasa, wao—hiyo halmashauri ya Wazee, wao walitambua ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Walijua jambo hilo. Hapa alikuwepo mkuu wao papa hapa akimwambia Yeye, "Tunajua ya kuwa U mwalimu umetoka kwa Mungu, kwa maana Uzima ule ule wa Mungu unatiririka ndani Yako." Mnaona? "Tunajua ya kwamba mafundisho Yako si Yako mwenyewe; ni ya Mungu, kwa maana Mungu anathibitisha jambo hilo." Mnaona? "Uzima wa Mungu unatiririka moja kwa moja ndani Yako." Sasa angalieni!

*Yesu akijibu akamwambia, Amin,. . .,* nawaambia, *Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu*. . . (Loo, jamani! "Usipojiunga na kanisa langu. . ." Loo, mnaona jinsi mnavyopotea? Mnaona, mnaona?)

Ndipo *Yesu—Yesu akijibu akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na*. . .*Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*

*Kilichazaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.*

*Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.*

*Upepo* unavuma *upendako*,. . . (Mnaona? Moja kwa moja tena. Mnaona? Akirudi. Mnaona?). . . *Upepo* unavuma *upendako, na sauti yake* huwezi kuisikia—kusikia *sauti yake, lakini hujui* mahali *unakotoka, wala* mahali *unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu* ambaye amezaliwa *kwa Roho.*

*Nikodemo akajibu, akamwambia, Yawezaje kuwa mambo haya?*

*Yesu akajibu, akamwambia, Je! wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?*. . . (Angalia pale, ndugu, D.D., Ph.D., L.L.D. Mnaona?), *na mambo haya* huyajui?

*Amin,. . ., nakuambia kwamba, Lile tulijualo twalinena, na lile tuliloliona twalishuhudia; wala ushuhuda wetu* nyinyi *hamwukubali*. . . (Tunayajua mambo haya. Tumeyaona; tunajua jambo hilo, wala hata hamwukubali ushuhuda wetu, mjiunga na kanisa. Mnaona?)

> *Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala hamsadiki, mtasadiki wapi niwaambiapo mambo ya mbinguni*?. . . (Sasa, sikilizeni jambo hili hapa. Sasa, angalieni!)
>
> *Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu*, aliye mbinguni.

Wazia jambo hilo. Mnajua wakati mmoja Yeye alisema, “Mnafikirije juu ya Kristo? Yeye ni Mwana wa nani?”

Wao wakasema, “Mwana wa Daudi.”

Akasema, “Basi kwa nini Daudi, katika Roho, anamwambia Yeye, ‘Bwana alimwambia Bwana wangu, “Uketi mkono Wangu wa kuume”’?” Awezaje kuwa Bwana Wake na Mwanawe? Hakuna mtu aliyemwuliza jambo lingine lo lote.

Katika Ufunuo Yeye alisema, “Mimi ni Shina na Mzao wa Daudi.” Mnaona? “Mimi ni Mzabibu na Tawi. Mimi ni mwanzo. Nilikuweko kabla ya mwanzo; nilikuwa mwanzo, na—na nilikuwa Mzao wake pia.”

Sasa, hapa Yeye alisema, “Hakuna mtu aliyeshuka kutoka Mbinguni, ila Mwana wa Adamu aliye sasa Mbinguni.”

Bibi fulani aliniuliza wakati mmoja, swali, nikasema, “Nijibu hili.”

Kasema, “Yesu alimwomba Nani katika bustani ya Gethsemane?”

Nikasema, “Yeye alikuwa akinena juu ya Nani wakati aliposema, ‘Hakuna mtu aliyepaa Mbinguni, ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni, yaani Mwana wa Adamu aliye—aliye sasa Mbinguni’?”

Huyu hapa, amesimama papa hapa juu ya nyumba akizungumza na Nikodemo, kisha akasema, “Mimi niko Mbinguni.” Hiyo ni kweli? Hebu tuliache jambo hilo hadi usiku wa leo, mnaonaje? Muda unaenda sana. Loo, jamani! Hebu tuwazie tu jambo hilo kwa muda kidogo alasiri ya leo.

Unaingiaje Kanisani? Kuzaliwa! Na nini? Pumzi ya Mungu!

> Nipulizie, nipulizie;
> Roho wa Mungu Aliye Hai, nipulizie.

Hilo ndilo ombi langu. Acha tu Roho Mtakatifu apulizie. Loo, jamani, nina hamu ya pumzi ya Mungu. Ni nini? Kutiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu, nikijua ya kwamba wakati nilipokiri kwanza, “Namwamini Yesu Kristo” . . . Naam.

Kisha kwenye imani yangu, natia nguvu, nguvu za kiungu. Halafu kwenye nguvu zangu, natia maarifa ya Neno. Kwenye maarifa yangu natia kiasi, kuweza kujitawala. Ninaupenda huo, “Nchi yangu ni yako . . . Tia taji nafsi yangu kwa kuweza

kujitawala . . . Kutoka bahari hadi bahari inayong'aa." Saburi. Loo, jamani! Kujaribiwa: usijali, Shetani atakujaribu na vitu hivyo.

Ninapanda ile ngazi sasa. Mnaona? Nimetia nguvu, maarifa, kiasi; sasa sina budi kutia saburi. Bado sina Roho Mtakatifu. Kisha baada ya kutia saburi, natia utauwa. Unajua huo ni nini? Kuwa kama Mungu. Ninatia huo. Sifanyi matendo mabaya; enenda kama Mkristo muungwana anavyopaswa kuenenda. Hebu hilo lisiwe la kuigiza. Kitu fulani ndani yangu, upendo wa Mungu unachemka tu . . . Mnaona, mnaona? Si kusema, "Mimi—mimi—mimi . . . Jamani, ningeweza kufanya jambo hilo, bali labda afadhali nisilifanye." Mnaona? A-ha; A-ha! Liko pale hata hivyo. Ni kuzaliwa. Nimezaliwa katika *hii*, katika *hili*, katika *hili*, katika *hili*, katika *hili*, katika *hili*, katika *hili*, halafu upendo wa Mungu, Kristo, anashuka na kutia muhuri hayo yote ndani yangu kwa ajili ya utumishi. Mnaona?

Basi anafanya nini anaponipa Roho Mtakatifu? Anakuweka kule nje peke yako katika mahali palipotengwa, anakutia alama. Mnaona? Wewe ni mtu tofauti basi. Wewe si wa ulimwengu tena (mnaona?), umevikwa tofauti. Unavalia nguo tofauti. Si nguo hii ya nje. La, la! Haikubidi kuwa mtu tofauti na wa kipekee, pamoja na ukosi uliopinduliwa, na vasi refu kama la sherehe. La, la! Hufanyi hivyo. Unavaa kama kawaida ya mtu kama . . . Vazi—vazi refu la kiroho ndilo tu kitu muhimu. Umevalishwa vazi la arusi. Wewe ni nini? Kama Yesu.

Angalia, Yeye alitiwa uvuli, na akageuka sura pale mbele yao. Na vazi Lake likang'aa kama jua. Huyo hapo, Yesu, Mungu akimweka Mwanawe mahali Pake. Mnaona? Halafu, akaja Musa. Kisha akaja Eliya. Basi Petro akasema, "Mwajua, ni—ni jambo zuri kuwa hapa." Unaona vile mwanadamu anavyokuwa? Loo, ya kimbinguni yalifanywa . . . Kasema, "Natujenge vibanda vitatu. Na tujenge kimoja kwa ajili ya Musa, na kimoja kwa ajili ya Eliya, na kimoja kwa ajili Yako."

Basi kabla hajamaliza kusema, Mungu akafunga tu jambo lote, kasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu. Katika mambo haya yote niliyomtaka Musa, na nikatoa amri kwa njia ya Musa, haki kwa njia ya manabii, Yeye ametimiza yote. Msikieni Yeye. Nitajiondoa sasa. Msikieni Yeye tu. Msikieni Yeye tu." Loo, jamani, ni jambo zuri jinsi gani.

Halafu, tunapotimiza masharti haya na kujaa wema wa Mungu na mambo ya Mungu, ndipo Roho Mtakatifu anaposhuka na kututia muhuri katika Ufalme. Msijali. Kila mtu atajua ya kwamba unaye Huyo. Hutakuwa na haja ya kusema, "Vema, Mungu atukuzwe, ninajua ninaye; nilinena kwa lugha. Mungu atukuzwe, ninajua ninaye; nilicheza katika

Roho wakati mmoja." Huna haja ya kusema kitu juu yake; kila mtu atajua unaye; Usijali. Yeye atajishuhudia Mwenyewe. Atatangaza jambo hilo kati ya watu.

Mungu awabariki. Ninafurahi sana kuwa pamoja nanyi asubuhi ya leo na kuwa na wakati huu wa ushirika. Sikilizeni! Maskini kanisa letu ni dogo, na hata hivyo hatuna nafasi ya kutosha kwa ajili ya watu wanaokuja hapa. Sisi si madhehebu. Sisi tunaamini na tunashiriki pamoja na kila madhehebu. Mnakuja tu hapa, kwa sababu kwamba mnataka kuja. Nanyi. . .Tunawapenda, na tunataka kila madhehebu, kila mtu. . .

Ninaamini ya kwamba kuna watu katika madhehebu hayo yote ambao ni Wakristo. Wao ni ndugu na dada katika Kristo. Kwa hiyo basi, hatuna masharti, hakuna kitu cha kujiunga nacho, hakuna la kufanya, bali uwe tu Mkristo.

Kama alivyozoea kusema E. Howard Cadle, "Hatuna sheria ila upendo, hatuna kitabu ila Biblia, hatuna kanuni ya imani ila Kristo." Na hiyo ni kweli. Njoo ukatutembelee. Tuna furaha ku-. . .Tunaamini Injili Yote, kila sehemu ya Neno. Tunaamini tu vile hasa. . .Hatuongezi jambo moja Kwake, kuondoa lo lote Kwake, kuongeza upuuzi wo wote wa kimadhehebu Kwake. Tunaliacha tu jinsi tu lilivyo. Naam. Nasi daima tunafurahi kuwapokea. Njoni mwe pamoja nasi mwezapo. Tunawaombea wagonjwa. Tunaamini kila kitu inachosema Biblia tufanye. Tunasahau "unyonge wetu, nyuma, nasi tunapiga mbio kuelekea mede ya wito mkuu."

Sasa, jambo moja zaidi. Mtaruhusu lisemwe? Siku iliyotangulia jana asubuhi. . .Mtaona kwenye—kwenye ubao wa matangazo kule nje ono. Nilipata ono. Ilikuwa kama saa 11, kama mke wangu kule nyuma ajuavyo, ama 12. Nilikuwa nimeamka. Tulikuwa tumeamka kuwatayarisha watoto kwenda shuleni. Ninapata haya mara kwa mara; nanyi nyote mnajua, kila mmoja wenu hapa, ya kwamba hayashindwi. Ni—ni makamilifu kabisa (mnaona?); hayashindwi.

Nami nilifikiri nilikuwa mtu mwenye furaha sana niliyepata kuona. Nilikuwa nimesimama kwenye jua, j-u-a, nami nilikuwa ni—nikihubiria Injili kusanyiko kubwa mno (nilitaka tu kuona kama yananaswa) ku—ku—kusanyiko kubwa mno. Nao walikuwa wameketi msituni, na miali ya jua ilikuwa inawaangazia, hapa tu na pale, wakiipata, wakilipata Neno.

Nami, kama kawaida, daima nachukua wakati mrefu sana, nawacheleweshа sana, nahubiri kwa muda mrefu sana. Na nikahubiri kwa muda mrefu sana, mpaka kusanyiko likawa na njaa ya chakula cha kawaida. Nao, wengine wao wakachoka, kwa hiyo waliamka tu wakatoka wakaenda kujipatia chakula, wakaanza kutoka nje. Nikasema, "Msitoke, msitoke."

Nilikuwa nina vipeo viwili nilivyotaka kufikia—nilivyotaka kufikia katika somo langu. Naye Bwana alikuwa amenipa hilo. Na mhubiri ye yote anajua wakati unajua kweli ni—Mungu amekupa hilo, unakuwa na shauku sana ya kuwaambia watu. Nami nilikuwa tu ninahubiri, "Charlie," kwa nguvu tu nilivyoweza kuhubiri, nikiyaelezea tu, mwajua, na kusema, "Mambo haya yote makuu. . .Hivi ndivyo Mungu anavyofanya, angalieni jambo hili. Yeye anatambua mawazo ya moyo. Ni nini? Neno," huku ninaendelea namna hiyo.

Ndipo lo, laiti ningalikumbuka niliyokuwa ninasema, somo langu lilikuwa nini. Siwezi kulikumbuka. Mnaona? Lakini nilikuwa ninahubiri tu, nami nilikuwa nikijiangalia nikifanya jambo hilo. Ndipo basi, nilipokuwa nimesimama pale nikitazama na kujiangalia mwenyewe nikilihubiri. . .Nami nilikuwa nikihubiria "ambaye asingeamini." Basi baada ya muda kidogo nikainuka, mwajua, kisha nikawaza, "Mungu atukuzwe." Nikasema, "Angalia mambo haya ya ajabu, na *hili*, *lile*. . ."

Moja kwa moja, nikaona watu wakianza kufanya kama kwamba walikuwa na njaa ya kawaida. Na kwa hiyo walikuwa na cha kutosha kiroho, kwa hiyo wakaanza kuondoka na wengine wao [Ndugu Branham anapiga miayo kutoa mfano—Mh.] wakaanza kuondoka. Nikawaza, "Kuna nini kwa kila mtu?" Na—nami nikaangalia na hapa walikuweko maskini wake na waume zao wanapita karibu nami, ndipo nikanyamaza; nikasema, "Hebu kidogo, marafiki, hebu kidogo. Mtarudi tena wakati vivuli vya jioni vitakapotua." Mnaona? Nikasema, "Mtarudi tena." Lakini, hebu niwape kipeo hiki cha kwanza. "Mambo haya yote niliyowaonyesha hutoka wapi? Yametoka wapi?" Nikasema, "Haya hapa. Yako kwenye Neno la Mungu. Hayo ni BWANA ASEMA HIVI, ahadi Yake, maana," nikasema, "ninyi nyote mnanishuhudia, mnashuhudia jambo hili, ya kwamba agizo langu ni, 'Kaa na Neno.'" Nikasema, "Ninyi nyote mna nini? Hivi hamwezi kulifahamu Neno? Hamna budi kulifahamu."

Ndipo mtu fulani akasema, "Jamani, ningetaka kula biskuti," na kadhalika namna hiyo.

Vema, niliwaza tu, "Vema, Mungu atukuzwe. Iwapo wanataka biskuti, na waende wakazichukue." Kwa hiyo ni—nikageuka; nikawaza, "Loo, lakini wajua nini? Vivuli vitatua baada ya kitambo kidogo. Mara moja." Kisha nikasema, "Halafu usiku wa leo, wakati kusanyiko hilo litakapokusanyika tena. . . Sasa, niliwawekea kipeo na kuwaambia ya kwamba mambo ambayo wameniona mimi nikiyafanya yanapatikana katika Neno la Mungu, si katika vitabu fulani vya kujibunia wala madhehebu fulani, yanapatikana katika Neno (mnaona?), kila sehemu yake katika Neno, maana nimeagizwa kufanya jambo hilo." Nikawaza,

"Wajua, kila mmoja wao atarudi usiku wa leo. Kwa hiyo hivi ndivyo nitakavyofanya: nitaliwekea msingi, kuliwekea msingi kwa namna fulani." Mnajua jinsi ninavyofanya jambo hilo katika nyakati hizi za kanisa na kadhalika, kusema niliyosema hapo awali. "Nitaliwekea msingi kwa Neno, halafu kipeo hiki kikubwa na cha ajabu sana. . . " Nikasema, "Utakuwa wakati wa jinsi gani. Mungu asifiwe." Nami nikajiona nikifanyika mdogo sana, ndipo nikasikia hiyo, "Mungu asifiwe." Nikajiona mwenyewe nikififia namna hiyo, nami huyu nimesimama pale.

Sasa, hii hapa fasiri yake. Mnaona? Jambo la kwanza nililofanya: Mambo ambayo yamefanywa yamekuwa ya kisiri kwa watu—karibu wote. Simaanishi Injili Yote na watakatifu wa Mungu, bali ninamaanisha kwa watu walio wengi sana. Nanyi hamtaki kamwe kuangalia ulimwengu, *Cosmos*, kama Ujumbe wa Mungu. Mnapoingia, mnasema . . .

Kama vile Boze alivyosema, "Daima nime-. . . " Kasema, "Niliota ndoto miaka kadha iliyopita ya kwamba Mu—Mu—Mungu angenituma Chicago na kuutikisa Chicago kwa utukufu wa Mungu."

Nikasema, "Joseph, Yeye tayari amefanya jambo hilo."

"Mbona," akasema, "wao hawajatikiswa tangu siku za Moody."

Nikasema, "Hilo . . . Mimi ninazungumza juu ya Kanisa. Hao ni chakula cha mizinga huko nje. Hao ni mavumbi tu ya ardhi; kundi hilo linalosongamana mitaani, na Mayezebeli waliojipodoa, na kila kitu . . . " Nikasema, "Hao ni huko nje. Hayo ni maloji makubwa ya kale na kadhalika yataporomoka na kuanguka mitaani huko." Nikasema, "Yeye ananena juu ya Kanisa. Kanisa limeona ufunuo wa Yesu Kristo ukidhihirishwa, nao wanautambua. Huenda wasiweko kumi na watano kutoka Chicago. Huenda wasiweko kumi katika kizazi hiki kutoka katika jiji zima la Chicago na kadhalika."

Ulipata kuwazia jambo hilo? Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, ambapo watu wanane waliokolewa. Ni wangapi waliotoka Sodoma? Mnaona ninalomaanisha? Nina shaka watakuwa wachache sana. Mnaona?

"Lakini Kanisa lenyewe limekwishapata mtikiso. Wao wametambua jambo hilo. Walijua Neno. Walilitambua Neno lilipokuwa likifanyika mwili, nao wakalishika. Sasa, angalieni jambo hilo kwa muda kidogo."

Sasa, na huu ujumbe wa kwanza, wakiisha kuuona, kila mtu aliufuata; kasema "Loo, Mungu atukuzwe. Loo, kama ningeweza kuona . . . *hili, lile*, na *linginelo*," nao wangeondoka moja kwa moja, jinsi ile ile walivyoingia. Mnaona? Na sasa,

wao wanafikiri, “Vema, sijui. Ungejiunga na wapi? Kama sitakuja pamoja na *hili*, itakuwa namna *hii*; nami nitafukuzwa nitoke *hapa*, nami sitakuwa na la kufanya *hapa*.”

Nao ndugu wanaketi na kusema, “Vema, ningefanyaje kama mimi...?” Mnaona pale? Wao hawatakaa muda mrefu wa kutosha waone Hilo ni Neno ambalo Mungu aliahidi sasa linadhihirishwa (mnaona?), nao wakaondoka. Bali msijali, vivuli vimekaribia sana. Mnaona?

Niliporudi kwenye huduma... Mnakumbuka usiku wa juzijuzi wa ujumbe alionipa huko nyuma nilipokuwa nikiweka jiwe la pembeni. Vile vile kabisa, kasema, “Fanya kazi...” Kasema, “Utakapotoka kwenye ono hili, soma 2 Timotheo 4.” Mnajua liko pale pale kwenye jiwe la pembeni—miaka thelathini na mitatu iliyopita. Kasema, “Fanya kazi ya mhubiri wa Injili. Timiliza huduma yako, maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi wenye masikio ya utafiti, watajiepusha na hadithi za uongo—watajiepusha na yaliyo Kweli na kuzigeukia hadithi za uongo.” Kama hilo halijatukia neno kwa neno.

Lakini kumbukeni basi, usiku wa juzijuzi wakati sikusoma yaliyosalia. Miaka thelathini na kitu ambayo nimehubiri kwenye maskani haya, hata wakati mmoja sikuenda mbali zaidi ya hapo, nami sijui ni kwa nini. Mara nyingi nimeshangaa, hata siku moja nikaona ambapo Yesu alitwaa Gombo na kuanza kusoma, ndipo akasoma nusu ya unabii, kisha akasimama, ndipo akasema (kule Kapernaumu), akasema, “Basi leo, unabii huu umetimizwa.” Kwa nini hakusoma yaliyosalia? Yanahusu kuja Kwake kwa pili. Mnaona?

Na pale ningesoma hayo bila kujua...Nilitwaa hilo, na ndilo hilo papo hapo mbele yangu kule Southern Pines, Carolina ya Kusini. Asubuhi hiyo, nikisimama pale nikizungumza na Joseph Boze, niliegemea kwenye upande mmoja wa motokaa [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.], nikalipata. Paulo alisema, “Mimi...Watu wote wamenichukia. Hakuna mtu aliye pamoja nami. Dema ameniacha, akiupenda ulimwengu huu wa sasa. Na mimi sasa...(angalia!) Naye mfua shaba ameonyesha ubaya mwingi kwangu.”

Angalia yale hapana budi Dema aliwazia. “Mbona, nimemwona Paulo akihubiri Injili na kuwaponya wagonjwa; na huyu hapa ameketi akiugua yeye mwenyewe, akiambatana na daktari, Luka, kila mara anapoenda, akiambatana na daktari, mtu anayehubiri Kiungu... Mbona, nilimwona akimpiga mtu upofu; kasema, ‘Bwana na akukemee, nawe utakuwa kipofu kwa muda’; halafu anamwacha mfua shaba

amfukuze mkutanoni. Nafikiri alipoteza nguvu za kumpofusha mtu. Hatimaye alipoteza nguvu za kuponya Kiungu. Mungu amemgeuka."

Sidhani Dema alienda ulimwenguni, maana Dema alikuwa wa... Mwajua historia yake, alitoka kwenye jamaa kubwa na tajiri; naye alitaka kuambatana na huo umati mwingine. Bali Paulo, maskini Paulo, ilikuwa ni nini? Mungu daima huacha huduma ifikie mahali kama hapo kisha anaitia taji. Yeye alimwacha Yesu afikie mahali (angalia pale!), ambapo Yeye aliweza kuwafufua wafu, ambapo angefanya lo lote alilotaka, kisha akamwacha askari wa Kirumi ang'oe ndevu kutoka usoni Mwake na [Ndugu Branham anatoa sauti ya kutema mate—Mh.] kumtemea mate usoni Mwake. Wakampiga kwenye...Wakamfunika uso kwa kitambaa na kusema, "Sasa, wajua, wao wananiambia ya kwamba wewe ni nabii..." Wote walisimama karibu wakiwa na mianzi yao na [Ndugu Branham anatoa mfano wa kumpiga Yeye—Mh.], wakampiga Yeye kichwani, wakasema, "Sasa twambie ni yupi aliyekupiga." Yeye alijua ni nani aliyempiga. Hakika alijua! Mnaona? Bali huduma yake ilikuwa karibu kutiwa taji. Daima inafikia mahali hapo ambapo inaonekana kana kwamba ni nyonge sana sana, imekaribia sana kwisha, ndipo Mungu anaitia taji. Loo, Bwana, na itendeke. Na itendeke, Bwana. Na tuinamishe vichwa vyetu.

> Nampenda, nampenda,
> Kwani alinipenda kwanza, (Sasa, mwabuduni;
> tumekuwa na mafundisho magumu!)
> Na kununua wokovu wangu mtini Kalvari.

Na tumwinulie Yeye mikono yetu sasa.

> Nampenda, (Naam, iweni katika Roho.
> Mnaona? Nampenda.] Nampenda,
> Kwani alinipenda kwanza,...

*Majina Ya Makufuru*, Vol. 8 No. 3
(*Blasphemous Names*, Vol. 3 No. 21)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Novemba 4, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1996 na Voice Of God Recordings.

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

Copyright notice

All rights reserved. This book may be printed on a home printer for personal use or to be given out, free of charge, as a tool to spread the Gospel of Jesus Christ. This book cannot be sold, reproduced on a large scale, posted on any website other than www.branham.org, stored in a retrieval system, translated into other languages, or used for soliciting funds without the express written permission of Voice Of God Recordings®.

For more information or for other available material, please contact:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org